

**TASFIDA KAMA MKAKATI WA UPOLE: UWIANO WA TASFIDA ZA  
KISWAHILI NA EKEGUSII**

**UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRAR -  
EAST AFRICANA**

**NA**

**FLORAH N. OMOSA**

**C50/84117/2012**



**A1500549A**

University of Nairobi Library Book

*Printed Feb, 2018*

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA  
KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJIYA SHAHADA YA UZAMILI  
KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**OKTOBA 2015**

## UNGAMO

Nakiri kuwa tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na hajawahi kuwasilishwa kwa utahini katika Chuo Kikuu cha Nairobi wala chuo kingine chochote ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika masomo ya Kiswahili.

Jina Florah N. Omosa

C50/84117/2012

Sahihi 

Tarehe: 19/11/2015

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwakwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu cha Nairobi

Jina: Dkt. Nyachae Michira

Sahihi 

Tarehe: 19.11.2015

Jina: Dkt. Prisca Jerono

Sahihi 

Tarehe: 23.11.2015

## **TABARUKU**

Tabaruku hii ni kwa mume wangu mpendwa Alfred Gichaba na watoto wangu Ruth, Sheila, na Linda.

Na

Wazazi wangu wapendwa Peterson Omosa na Bathsheba Moraa.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa na kwa dhati ya moyo wangu namshukuru mwenyezi mungu muumba kwa uhai, hekima, neema na fadhili zake zisizokadirika katika mchakato wa maandalizi ya tasnifu hii.

Ningependa, kutoa shukuruni zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Nyachae Michira na Dkt. Prisca Jerono kwa ukarimu wao na kujitoa katika kazi nzima kwa ushauri na kunipa mwongozo jinsi ya kuifanya kazi hii. Kiwango cha upendo na mwongozo walichokionyesha hakiwezi kupimika wala kulipwa. Hakika mchango wao hautasahaulikakamwe.

Nawashukuru wahadhiri wote katika Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Nairobi kunidahili kwa ajili ya masomo ya shahada ya uzamili. Mafunzo, maelekezo na ushauri wenu ulinitia moyo kukamilisha kazi hii. Shukrani zangu za pekee ziwafikie Profesa John Habwe, Profesa Kineene wa Mutiso, Profesa Mwenda Mbatia, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Iribemwangi, Dkt. Amiri Swaleh, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Ayubu Mukhwana Dkt Evans Mbuthia na Bwana Mungania. Nawaombea Baraka za Mwenyesi Mungu.

Nitakuwa mtovu wa fadhila iwapo sitawataja mume wangu mpendwa pamoja na watoto wangu. Ukarimu na uvumilivu wenu umekuwa motisha kuu kwangu kuiendeleza na kuikamilisha kazi hii. Bila msaada wenu singekamilisha kazi hii. Mungu awape heri kulingana na mapenzi yake mnapoendelea kulisukuma gurudumu la maisha.

Siwezi kuwasahau wazazi wangu wapendwa katika shukrani hizi. Babangu Peterson Omosa na mamangu Bathsheba Moraa. Asante kwa kuonyesha imani katika uwezo wangu. Bila juhudi zenu za kunipeleka shule, singekuwa na fursa ya kuifanya kazi hii. Nawaombea Baraka na siha njema.

Siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu tulioshirikiana katika bahari ya masomo ya uzamili. Ushauri wao ulinitia hamu ya kuendeleza na hata kuikamilisha kazi hii. Wenzangu hawa ni pamoja na Evelyne Khanyange, Julita Nanjala, Gladys Kinyua, Peter Kilonzo, Judy Kemunto, Rose Nyamemba, Paul Sito, Rose Nyaga, Diana Osango, Lydia Shiviya, Queene Ndodi, Hadson Nyandhiwa, Damaris Otuoma, Regina Gitau, Mutahi Miricho na Zani mwa Zani. Daima nitawakumbuka kwa hisani yenu.

Mwisho, siwezi kuwasahau ndugu zangu, Orpha Gesare, Simon Nyagaka Grace Nyarangi na Haron Magati kwa kunitia shime ya kuendelea na masomo haya.

Shukrani ziwafikie wale wote walionisaidia kukamilisha kazi hii. Mola awape dua njema.

## IKISIRI

Tasfida hutekeleza majukumu muhimu katika mawasiliano ya watu ya kila siku. Tasnifu hii ni uchunguzi wa uwiano wa tasfida za Kiswahili na Ekegusii kama mkakati wa upole. Uchunguzi huu ulinuia kubainisha hali zinazozua matumizi ya tasfida, mchango wa tasfida katika kuendeleza upole katika jamii na kudhihirisha uwiano tasfida za Kiswahili na Ekegusii. Nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1978, 1987) ilitufaa katika uchunguzi wa tasfida. Ilibainika kwamba ukosefu wa upole ni mwiko katika jamii. Tasfida hutumika kupunguza vitendo vinavyotishia uso na kudumisha upole miongoni mwa wanajamii katika mawasiliano. Tunadai kwamba tasfida hazitumiki tu kama njia ya kukwepa dhana au mada zisizotajwa hadharani, bali pia ni jambo la kimsingi la kupunguza mitafaruku na migongano baina ya wanajamii. Pia ni chombo chenye nguvu kinachotumika kuongeza upole na kuhifadhi nyuso za kibinafsi na nyuso za hadharani kwa washiriki wa mawasiliano. Hutumika kuimarisha mahusiano mema baina ya wanajamii katika mawasiliano. Kwa hakika katika mitagusano ya kila siku, lazima pawe na upole ili kudumisha mawasiliano. Aidha kutosema taarifa kwa njia ya moja kwa moja ni njia ya kuwa mpole zaidi katika mawasiliano.

## YALIYOMO

UNGAMO.....	ii
TABARUKU.....	iii
SHUKRANI.....	iv
IKSIRI.....	vi
YALIYOMO.....	vii
SURA YA KWANZA .....	1
MSINGI WA UTAFITI.....	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.1.1 Lugha ya Ekegusii.....	3
1.1.2 Lugha ya Kiswahili .....	3
1.2 Tatizo la utafiti.....	5
1.3 Madhumuni ya utafiti.....	6
1.4 Nadharia tete .....	7
1.5 Sababu za kuchagua mada.....	7
1.6 Upeo na mipaka.....	7
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada .....	8
1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu upole.....	10
1.8 Msingi wa nadharia .....	11
1.8.1 Vitendo vinavyotishia uso.....	12
1.8.2 Uso hasi.....	14
1.8.3 Uso chanya.....	14
1.8.4 Mkakati wa upole hasi.....	15
1.8.5 Mkakati wa upole chanya.....	16
1.8.6 Mahitaji ya uso .....	17
1.8.7 Mikakati ya kuheshimu uso .....	18
1.8.8 Upole chanya.....	18
1.8.9 Upole hasi.....	19
1.8.10 Mkakati wa kuwa kwenye rekodi .....	19
1.8.11 Mkakati wa kuwa nje ya rekodi .....	21
1.9 Njia zautafiti.....	21

1.9.1 Mbinu za ukusanyaji data.....	22
1.9.2 Mbinu za uchanganuzi na uwasilishaji wa data .....	22
<b>1.10 Hitimisho.....</b>	<b>22</b>
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>23</b>
<b>HALI ZINAZOZUA MATUMIZI YA TAFIDA .....</b>	<b>23</b>
<b>2.1 Utangulizi.....</b>	<b>23</b>
<b>2.2 Dhana ya tasfida.....</b>	<b>23</b>
<b>2.3 Kanuni za matumizi ya tasfida .....</b>	<b>24</b>
2.3.1 Kanuni ya urefu.....	24
2.3.2 Kanuni ya kuinga uso .....	25
<b>2.4 Historia na maendeleo kuhusu tasfida.....</b>	<b>25</b>
2.4.1 Tasfida chanya na hasi .....	26
2.4.2 Tasfida za desturi na zisizo za desturi.....	26
2.4.3 Tasfida ng'amuzi na tasfida ng'amuzibwete.....	27
2.4.4 Tasfida za misimu na tasfida endelevi.....	28
2.4.5 Tasfida za kitaaluma.....	28
2.4.6 Tasfida za anatomia.....	29
<b>2.5 Mahusiano miongoni mwa wanajamii .....</b>	<b>29</b>
2.5.1 Tofauti za kijinsia baina ya wanajamii.....	30
2.5.2 Tofauti zaumri baina ya msemaji na msikilizaji .....	30
2.5.3 Hadhi ya msemaji na msikilizaji.....	31
<b>2.6 Tofauti ya kazi.....</b>	<b>31</b>
<b>2.7 Tofauti za kidini .....</b>	<b>32</b>
<b>2.8 Hali za magonjwa miongoni mwa wanajamii .....</b>	<b>32</b>
<b>2.9 Hali ya kifo.....</b>	<b>33</b>
<b>2.10 Vitendo vya kujamiiana .....</b>	<b>33</b>
<b>2.11 Taka ambazo hutoka mwili wa binadamu.....</b>	<b>34</b>
<b>2.12 Sehemu za mwili.....</b>	<b>34</b>
<b>2.13 Sherehe mbalimbali .....</b>	<b>35</b>
<b>2.14 Hitimisho.....</b>	<b>35</b>
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>37</b>
<b>MCHANGO WATASFIDA KATIKA KUENDELEZA UPOLE .....</b>	<b>37</b>



<b>3.0 Utangulizi.....</b>	<b>37</b>
<b>3.1 Upole.....</b>	<b>37</b>
<b>3.2 Uhusiano baina ya tasfida na upole.....</b>	<b>38</b>
<b>3.3 Mtazamo wa upole kama kaida ya kijamii.....</b>	<b>38</b>
3.3.1 Upole kama mkakati wa mazungumzo .....	39
3.3.2 Kanuni ya mkataba wa mazungumzo.....	40
3.3.3 Mtazamo wa kuokoa uso.....	41
<b>3.4 Uchanganuzi wa data.....</b>	<b>41</b>
<b>3.5 Hitimisho.....</b>	<b>60</b>
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>61</b>
<b>UWIANO KATIKA TASFIDA ZA KISWAHILI NA EKEGUSII.....</b>	<b>61</b>
<b>4.0 Utangulizi.....</b>	<b>61</b>
<b>4.1Tasfida za Kiswahili na Ekegusii.....</b>	<b>61</b>
4.1.1 Tasfida za kujamiiiana.....	62
4.1.2 Tasfida za sehemu za siri za mwili.....	63
4.1.3 Tasfida za kumtaja mke .....	65
4.1.4 Tasfida za ujauzito .....	66
4.1.5 Tasfida za mapenzi.....	67
4.1.6 Tasfida za majina ya kijamii .....	67
4.1.6 Tasfida za mahusiano .....	68
<b>4.8 Hitimisho.....</b>	<b>72</b>
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>73</b>
<b>HITIMISHO.....</b>	<b>73</b>
<b>5.0 Utangulizi.....</b>	<b>73</b>
<b>5.1 Muhtasari wa matokeo .....</b>	<b>73</b>
<b>5.2 Mapendekezo.....</b>	<b>76</b>
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>77</b>
<b>VIAMBATISHO .....</b>	<b>80</b>
Data ya uchanganuzi I: Nyimbo za harusi za Kiswahili .....	80
Data ya uchanganuzi II: Nyimbo za harusi za Ekegusii.....	86

## SURA YA KWANZA MSINGI WA UTAFITI

### 1.1 Utangulizi

Utafiti huu unahusu uwiano wa tasfida za Kiswahili na Ekegusii kama mkakati wa upole. Tasfida ni chombo muhimu katika lugha ambacho kina majukumu muhimu katika mawasiliano ya watu ya kila siku. Katika mawasiliano, tasfida huongeza upole na kuhifadhi nyuso za watu. Ili mawasiliano yoyote yaweze kufaulu, upole hauwezi kuepukika. Upole ni utumiaji wa lugha kwa namna ambayo haiathiri watu wengine. Ni kuonyesha adabu njema na kushugulikia mahitaji ya wanajamii ya heshima. Upole hutumikaili kuinga uso na kuepukana na hisia hasi. Tasfida ni kipengele cha lugha kinachotumika kudhihirisha upole kwa lengo la kufanikisha mawasiliano.

TUKI (1990) inaeleza kuwa lugha ni mfumo wa sauti zinazotumiwa na watu wa jamii fulani wenye utamaduni unaofanana. Aidha lugha inayotumiwa na watu katika jamii ndiyo hasa hubeba utamaduni wa watu hao. Kwa hivyo jamii fulani huwakilishwa na lugha yake na matumizi ya lugha katika jamii hutegemea utamaduni wa watu hao. Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa tasfida ni mbinu ambayo watu hutumia lugha safi ili maneno machafu yasitumike. Hivyo humwezesha mzungumzaji kusema dhana chafu hadharani bila kuchukiza au kufanya moyo wa msikilizaji au msomaji uchafuke. Mfano: kufa- kufariki, kuzaa- kujifungua.

Tasfida ni zao la shughuli za kijamii ambazo watu hushiriki kila siku. Katika hali hii ya ushirikiano na mitagusano ya kila siku, inawabidi wanajamii kutumia maneno ambayo hufanya mawasiliano yasivunjike. Kila jamii ina maneno fulani ya miiko ambayo hayasemwi hadharani. Wamitila (2003:194) anadai kwamba tasfida ni matumizi ya maneno ya kupunguza ukali au uzito fulani. Badala ya kutumia lugha inayoudhi au matusi, mzungumzaji hutumia lugha inayoficha makali hayo. Anaendelea kuelezea kuwa hii ni mbinu inayotumiwa katika jaribio la kutaja mambo yasiyokubalika kwa njia inayokubalika au hutumika kupunguza makali ya jambo linalosemwa.

Tasfida huumbwa na tamaduni za jamii. Hii basi ni mbinu mojawapo ya lugha ambayo hutumika kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii, kwani hupitisha amali na mambo ambayo jamii inayathamini. Harry (1954) anasema kuwa lugha huashiria mfumo wanajamii husika, kwa hivyo kuna uhusiano kati ya lugha na utamaduni. Kila utamaduni huwa na mambo ambayo hayazungumzwi wazi. Katika matumizi ya lugha, wazungumzaji na wasikilizaji wa lugha hujaribu kukwepa mambo ambayo hayazungumzwi wazi na hivyo wanaonekana kutumia lugha nzuri kiasi katika miktadha tofauti kulingana na mazingira ambayo wamo. Ni dhana ambayo humaanisha kuzungumza kwa usemi usiodhuru. Gatambuki (2009) akimrejelea Enright (1995), Allan na Burridge(1991) wanasema kwamba tasfida ni kutumia maneno mazuri yanayopendeza, matamu na yenye nakshi ya kuvutia na kuto sema maneno moja kwa moja ili kukinga uso wa watu wengine katika mazungumzo. Hivyo mzungumzaji ana jukumu la kutumia maneno ya upole anapowasiliana na msikilizaji wake.

Tasfida ni mojawapo ya kategoria za muktadha. Muktadha ni hali inayomzunguka mtu anapoitumia lugha na huathiri matumizi ya lugha. Ni hali mbalimbali zinazofungamana na utamaduni ulioko. Aidha ni mambo ambayo yanayoizunguka lugha na hueleweka katika hali mbalimbali kama vile elimu awali, muda na mazingira yenyewe. Muktadha ni muhimu katika ufafanuzi wa maana na uwezo wa kuelewa. Matumizi yoyote ya huwa lugha hayana maana yoyote mpaka pale yanapofungamanishwa katika muktadha maalum. Hufanya lugha kueleweka bayana pasina utata wowote. Brown na Levinson (1983:5) wanasema kwamba muktadha huathiri matumizi na uteuzi wa msamiati katika kujenga maana kwa lengo la kukuza na kuendeleza mawasiliano. Muktadha ni muhimu kuzingatiwa kwa sababu msemaji husema anachokisema wakati huo wa usemi. Inambidi msemaji azingatie vipengele vya kimuktadha kama vile hali, wakati na mahali patakapotolewa usemi na uhusiano wake na msikilizaji wake. Mzungumzaji ana jukumu la kuteua maneno yasiyodhuru anapowasilisha ujumbe. Lugha ya binadamu huwasilisha maana kupitia kwa mawasiliano. Msemaji hutumia maneno ambayo yana upole ili kuokoa uso wa msikilizaji.

### **1.1.1 Lugha ya Ekegusii**

Lugha ya Ekegusii ni ya asili ya Kibantu. Kazi ya Guthrie (1947-67, 1970/71), Nurse (1985) na Greenberg (1966) zinaonyesha kwamba barani Afrika mna makundi manne makuu ya lugha ambayo ni: Nile -Sahara, Khoisan, Niger-Kordofania na Kiafro-Asia. Lugha za Kibantu zimeanishwa katika kundi la Niger-Kordofania. Lugha hizi hasa huzungumzwa kwenye maeneo ya Afrika ya Kati na Afrika Mashariki. Nchini Kenya lugha za kibantu zimeanishwa katika makundi mawili makuu kimaeneo ambazo ni: lugha za Kibantu za maeneo ya magharibi mwa Kenya na za maeneo ya mashariki mwa nchi. Ekegusii ni lugha inayoorodheshwa katika kundi la magharibi ikiwa na uhusiano wa karibu sana na lugha nyingine kama vile Kikuria, Kibasuba na baadhi ya lahaja za Kiluhya.

Lugha ya Ekegusii ina lahaja mbili. Kuna lahaja ya Maate inayozungumzwa kwenye maeneo ya Bogirango kusini na baadhi ya sehemu za Bonchari na lahaja ya Rogoro inayozungumzwa katika maeneo ya Nyaribari, Bobasi, Bogetutu na baadhi ya sehemu za Bogirango kaskazini. Katika kazi hii tutarejelea lahaja ya Rogoro kwani ndiyo lahaja rasmi (Bosire 1993:1) na Mecha (2006). Katika utafiti huu tunazingatia Kiswahili sanifu kwa kuchunguza tasfida za Ekegusii ambacho wazungumzaji wengi wa Ekegusii pia huzungumza Kiswahili.

### **1.1.2 Lugha ya Kiswahili**

Kulingana na Guthrie (1971), Kiswahili ni lugha ya kibantu. Nchini Kenya lugha hii imeanishwa katikakundi la lugha za kibantu za pwani mwa nchi. Whitely (1969) naye pia anadai kwamba neno Swahili lina asili yakekatika Kiarabu lenye maana pwani. Hata hivyo Kiswahili ni lugha ya kibantu ambayo chimbuko lake ni upwa wa Afrika mashariki licha ya kuwepo madai mengi kuhusu chimbuko lake. Sifa moja kuu inayozitambulisha lugha za Kibantu ni kuwa nomino zake hupangwa kwa makundi yanayoitwa ngeli ambayo katika sentensi huonyesha upatanisho wa kisarufi. Hata hivyo lugha hizi zina baadhi ya tofauti zinazojitokeza katika viwango vyote vya kiisimu yaani, fonolojia, mofolojia na sintaksia.

Lugha ya Kiswahili ilianishwa na Guthrie (1948) kama lugha ya kibantu ya kundi la G. Nchini Kenya Kiswahili kilibainishwa kuwa na lahaja kumi na nane. Baadhi yazo ni Kiunguja, Kimvita, Kiamu, Kimtang'ata miongoni mwa lahaja zingine. Utafiti wetu unalenga Kiswahili sanifu ambacho kilisanifishwa kutokana na lahaja ya Kiunguja. Kiswahili ni lugha inayozungumzwa na watu wengi. Bakari (1982) anaunga mawazo haya kwa kueleza kuwa Kiswahili ndiyo lugha ya kiasia inayozungumzwa na watu wengi zaidi ya zote katika Afrika ya kati na ya mashariki. Kwa mujibu wa Massamba (1999), zaidi ya watu milioni sitini ulimwenguni hutumia lugha ya Kiswahili. Chimera (1998) naye anadai kwamba ni zaidi ya watu milioni mia moja arobaini huzungumza lugha ya Kiswahili.

Iribemwangi (2011) na Okombo (2001) wameitaja lugha ya Kiswahili kama Lingua Franca, yaani lugha ya mawasiliano mapana na inayotumiwa na watu ambao lugha zao za kwanza ni tofauti. Ni lugha inayotumiwa katikanyanjanja za biashara pamoja na mawasiliano katika Afrika yamashariki, Afrika ya kati na Afrika kusini. Mbaabu (1991) na Chimera (1998) pia wameitaja kama lugha inayozungumzwa katika eneo la kusini mwa Omani na kule Uajemi.

Lugha hii imekuwa ikitumika kama lugha ya taifa nchini Kenya. Kiswahili hutumika katika shughuli rasmi kama vile shughuli za elimu, biashara na bungeni. Isitoshe ni lugha inayofundishwa hata vyuo vikuu na ni somo la lazima katika shule za msingi na za sekondari.

Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanaelezea kuwa inatahiniwa katika mitihani ya kitaifa katika shule za msingi nazi upili za umma katika nchi za Afrika mashariki. Pia ni somo linalofundishwa hata nje ya bara la Afrika kama vile Asia, Marekani na Ulaya. Lugha ya Kiswahili inatambuliwa kama lugha ya kimataifa kwa sababu inatumika katika shughuli za kisiasa, kidini na kibiashara na katika ngazi za kimataifa. Nchini Kenya baadhi ya vituo vya redio na televisheni hupeperusha matangazo yao kwa lugha ya Kiswahili.

Lugha hizi ni muhimu kwa sababu uchunguzi wetu unajikitakwa kurejelea tasfida za Kiswahili na Ekegusii. Kwa kuzilingasha tutakuwa tunaelewa jinsi jamii hutumia tasfida

ili kukuza mahusiano na mitagusano ya kila siku. ‘Uso’ pia ni muhimu kwa sababu kila binadamu hupenda kuhimiliwa.

Mahusino baina ya watu ni jambo muhimu katika jamii. Ili kudumisha mahusiano haya, watu huwasiliana kwa njia ya kutowavunjia wengine heshima. Katika hali hii mzungumzaji analazimika kutambua ni lipi linalofaa zaidi kusema, anachokisema au kusema kusudi aepukane na kupujua uso. Kuna baadhi ya maneno katika jamii ambayo hutumika kukuza heshima, mitagusano na ushirikiano miongoni mwa watu. Aidha kuna baadhi ya maneno yakitumika huweza kuathiri mawasiliano. Ili pawe na mawasiliano bora, mzungumzaji sharti ajiepushe na matumizi ya maneno yanayochukiza au yanayotishia uso, yaani atumie maneno ya adabu na heshima ambayo ni tasfida. Uteuzi na upangaji wa maneno yafaayo kutumika ni njia ya kudumisha heshima. Kwa mfano katika Ekegusii, neno ‘*enyonga*’ lenye maana makalio hutumiwa pasina kuvuruga mawasiliano. Hii ni kwa sababu linatumika jinsi lilivyo katika muktadha wowote licha ya kuonekana kuwa ni neno la aibu. Katika Kiswahili neno ‘makalio’ hutumika badala ya neno ‘*matako*’ kwa sababu lina upole kiasi. Katika Ekegusii, msemaji anapoashiria ugonjwa wa ukimwi, anaweza kusema ‘*enyamoreo*’ yenye maana ugonjwa unaokondesha. Tasfida hii imebuniwa ili kutopujua uso wa muathiriwa. Kuna maneno ambayo ni ya miiko katika lugha zote hasa yanayohusu sehemu za siri na kujamiiana. Hata hivyo si maneno yote ambayo yanaweza kuwa miiko katika lugha zote. Hii ni kwa sababu kile kinachotambulikana kuwa mwiko katika lugha hii, huenda si mwiko katika lugha nyingine.

## 1.2 Tatizo la utafiti

Kazi za wataalam mbalimbali zimeonyesha kwamba kuna matumizi ya tasfida katika lugha zote ulimwenguni. Buliba, Njogu na Mwihaki (2006) wakizungumzia kuhusu mwingiliano wa lugha wanasema kwamba kuna uhusiano kati ya lugha, jamii, utamaduni na mazingira. Lugha ni sehemu ya utamaduni wa jamii nakila jamii ina utamaduni. Lugha katika jamii hudhihirisha maadili na thamani ya jamii hiyo. Mbali na kuwasilisha maana, lugha pia inahusishwa na kujitambulisha kwa wanajamii ambao hushirikiana kutumia lugha hiyo. Franz (1978) anaeleza kuwa tasfida huumbwa na

utamaduni ambao huwasilisha lugha ya jamii husika. Illuman (2005) anaeleza kuwa kila utamaduni huwa na mambo ambayo hayazungumzwi wazi ambayo ni miiko. Mwiko ni chochote au mambo ambayo yamekatazwa katika jamii kwa sababu za kidini au za kiutamaduni. Katika matumizi ya lugha, wasemaji na wapokezi wa lugha hujaribu kukwepa mambo yanayohusu miiko. Ukwepaji huu hujikita kwa kutumia lugha inayoonekana kuwa nzuri katika miktadha tofauti ambayo huitwa tasfida.

Wanajamii katika mitagusano yao ya kila siku hutumia maneno ya upole. Wazungumzaji wa asili ya Ekegusii pia hutumia maneno ya upole. Baadhi ya tasfida katika hali ya kawaida katika lugha zingine huwa hazina upole na watu huzitumia bila uchukivu wowote wala kuvuruga mitagusano. Hali hii ndio imetupa msukumo wa kutaka kujua ni kwa kiwango gani tasfida huchungia upole huu. Aidha tunataka kuchunguza ni hali gani zinazosababisha kuwepo kwa matumizi ya tasfida. Tunataka kulinganisha tasfida za Kiswahili na Ekegusii ili tuone iwapo kuna tofauti kubwa kati ya tasfida hizo na iwapo tofauti hizo zinaathiri mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji wa Ekegusii na Kiswahili. Katika utafiti huu tutachunguza upole kwa kuzingatia matumizi ya tasfida za Kiswahili na Ekegusii. Kwa ujumla tunataka kueleza upole, na kuainisha tasfida zinazojitokeza katika matumizi ya lugha hizi mbili. Kwa kutambua upole huu itakuwa ni hatua muhimu ya kudumisha mahusiano na mitagusano miongoni ya wanajamii.

Uchunguzi huu utakuwa wa manufaa katika kushauri jamii kuwa na uelewa wa matumizi ya tasfida za lugha nyingine nakujua ni tahadhari zipi wanapaswa kuchukua katika kutumia tasfidazalugha nyingine. Hii ni kwa sababu neno laweza kuwa tasfida kwa lugha moja ilhali katika lugha nyingine si tasfida. Vile vile neno katika lugha moja ambalo ni la mwiko laweza kutajwa vile lilivyo katika lugha nyingine licha ya kuwa ni la mwiko katika lugha hiyo. Pia utafiti huu utakuwa ni msingi bora wa kuboresha mahusiano, kuendeleza na kuhifadhi lugha za jamii.

### **1.3 Madhumuni ya utafiti**

Utafiti huu unanuia kutekeleza yafuatayo:

- (a) Kubainisha hali zinazozua matumizi ya tasfida katika Kiswahili na Ekegusii.
- (b) Kujadili jinsi mikakati ya tasfida huendeleza upole katika Kiswahili na Ekegusii.
- (c) Kudhihirisha uwiano uliopo baina ya tasfida za Kiswahili na Ekegusii.

#### **1.4 Nadharia tete**

Utafiti huu unatarajia matokeo yafuatayo kutokana na malengo yake:

- (a) Hali ambapo tasfida za Kiswahili na Ekegusii hutumika si bayana.
- (b) Mikakati ya tasfida huchangia kuendeleza upole katika Kiswahili na Ekegusii.
- (c) Tasfida za Kiswahili na Ekegusii hukaribiana kwa kiwango kikubwa.

#### **1.5 Sababu za kuchagua mada**

Tasfida ni kipengele muhimu cha lugha ambacho hupatikana na kutumika katika lugha zote ulimwenguni. Lugha hutumika kuashiria mfumo wa jamii husika. Harry (1954) anasema kuwa lugha inayotumiwa na watu wote katika jamii ndiyo hasa hubeba utamaduni wa watu hao. Kwa hivyo kuna uhusiano baina ya lugha na jamii. Aidha upole hutumika miongoni mwa wanajamii kwa lengo la kufanikisha mawasiliano. Tumechagua mada hii kwa sababu tunataka kujua hali zinazozua matumizi ya tasfida katika lugha za Kiswahili na Ekegusii. Aidha tunataka kudhihirisha uwiano uliopo baina ya tasfida za lugha za Kiswahili na Ekegusii. Uteuzi wa mada hii vile vile umechochewa na malengo yake katika kukuza mahusiano, mitagusano na mwingiliano miongoni mwa wanajamii kwa kuwa kujua lugha sio tu kujua sarufi bali ni kujua kuhifadhi uso.

#### **1.6 Upeo na mipaka**

Kazi hii tunanua kudhihirisha uwiano uliopo baina ya tasfida za Kiswahili na Ekegusii katika kufanikisha mawasiliano. Tunajikita katika nyimbo tano za harusi za Ekegusii na nyimbo tano harusi za Kiswahili. Utafiti huu wetu hata hivyo hautaweza kushughulikia tasfida zote za lugha hizi kwa sababu tasfida ni nyingi katika kila lugha. Kwa hivyo tunashughulikia tasfida za Kiswahili na Ekegusii.



## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Hata ingawa mengi yameandikwa kuhusu tasfida, ikumbukwe kuwa kila lugha ina tasfida zake na tasfida hizo hutumiwa kwa njia ya kipekee. Kwa kuwa tutashugulikia tasfida hizo kwa kuzingatia lugha za Kiswahili na Ekegusii, tutarejelea yaliyoandikwa kuhusu tasfida na ulinganishi wa tasfida za lugha mbalimbali za kibantu na Kiswahili.

Hymes (1964) akimnukuu Nade (1954), Wardhaugh (2002) anaeleza kuwa Wanupe wa Afrika magharibi ni mojawapo ya watu wapole ulimwenguni kwa kufanya uteuzi mwafaka wa maneno yanayofaa zaidi badala ya kutaja maneno moja kwa moja kama vile yalivyo kwa mfano sehemu nyeti za mwili. Aidha kulingana na kazi yake, ni jambo muhimu kwa mzungumzaji kuteua maneno yasiyomvunjia heshima msikilizaji wake ili kufanikisha mawasiliano.

Katamba (1985) anaeleza kuwa tasfida ni neno ambalo hutumika kufafanua lugha, mawazo na dhana ambazo hupunguza uchukivu wa utamaduni wa jamii au kundi lolote la watu. Kazi hii itachangia pakubwa katika utafiti huu wetu kwa kuwa inatuwezesha kufafanua tasfida.

Leech (1983) anaeleza tasfida kama usemi unaorejelea hali chukivu na masuala nyeti katika jamii kwa hali bora kuliko yalivyo. Anadai kwamba tangu zamani kulikuwepo mijadala ambayo haifurahishi kwa wengine na kwa hivyo iliwabidi wanajamii kutafuta mbinu ya kukwepa mijadala hiyo. Mijadala hiyo ni pamoja na ngono, kifo, magonjwa na vitendo tofauti vya mwili wa mwanadamu miongoni mwa mijadala mingine. Anaendelea kuelezea kuwa watu hutumia tasfida ili kuondoa maana hasi. Alitambua kwamba tasfida hutokea katika viwango vyote vya kijamii.

Mutiso (2005) alichunguza maneno ya miiko ambayo hutumiwa katika lugha ya Kikamba hasa katika kumdunisha mwanamke, ameshugulikia jinsia ya kike kwa kulinganisha na jinsia ya kiume kwa kuonyesha jinsi jinsia moja imedhalilishwa. Uchunguzi huu haukujikita katika ulinganishi wa tasfida. Ulifikita sana katika jinsia. Kazi yetu inazingatia nafasi ya tasfida kama njia moja ya mkakati wa upole.

Njeri (2007) alichunguza tasfida katika mazungumzo kuhusu virusi vya ukimwi miongoni mwa jamii ya Wakikuyu. Anadai kwamba wakati mwingine tasfida hukwamiza mawasiliano hasa pale ambapo msemaji na mpokeaji ujumbe wanatofautiana kiumri, uana na kazi wanazozifanya. Anaendelea kueleza kwamba ingawa tasfida hutumika kupunguza athari hasi, baadhi ya tasfida zingali na athari hizo kwa uso. Katika uchunguzi wake alitumia nadharia ya Pragmatiki leksika ambayo ni tofauti na nadharia tunayoitumia. Uchunguzi wetu unatumia nadharia ya upole.

Wambua (2009) alichunguza tofauti zamatumizi ya kilahaja na mitazamo ya leksika za miiko na tasfida katika jamii ya Wakamba. Alitofautisha jinsi mitazamo tofauti inavyojitokeza katika matumizi ya leksika, miiko na tasfida kwa lahaja mbili za lugha ya kikamba. Uchunguzi wake ulijikita katika kulinganisha lahaja tofauti za lugha moja bila kuhusika na lugha nyingine. Katika kazi yake aligundua kuwa kila lahaja ina tasfida zake. Kazi yake ni tofauti na yetu kwani kazi yetu inazingatia kuhusisha Ekegusii na Kiswahili.

Mukaria (2011) alihusika na kuchunguza misamiati ya miiko na tasfida katika lahaja ya Kiiigembe. Katika kazi yake alichunguza jinsi wanaume wanavyosawiriwa katika matumizi ya misamiati ya miiko na tasfida. Uchunguzi huu ulijikita katika jinsia na matumizi ya tasfida. Aliainisha aina tofauti za tasfida na kutathmini jinsi ubabedume unavyojidhihirisha katika misamiati ya miiko na tasfida. Alibainisha jinsi tasfida hutumika kuinua jinsia ya kiume na kudhalilisha jinsia ya kike.

Nguti (2012) alichunguza matumizi ya tasfida za nyumbani katika lugha ya Kikamba. Katika uchunguzi wake alijikita sana katika muktadha wa nyumbani huku akizilinganisha tasfida za Kikamba na lahaja ya Kimvita. Alizianisha pia aina za tasfida. Ingawa kazi hii yaelekea kuwa karibu na yetu, sisi tunalinganisha tasfida za Ekegusii na Kiswahili sanifu hasa kwa kuangazia nafasi ya tasfida kama mkakati wa upole.

Leech (1983) ametalii maswala ya tasfida na kueleza kuwa tasfidani kipengele cha lugha am acho hutokea katika viwango vyote vya kijamii. Alieleza tasfida kama ile hali ya kutoa maana hasi na kutia maneno urembo au nakshi ili yaonekane kuwa ya kupendeza. Maelezo haya yatakuwa ya manufaa kwetu kwani yatatuelekeza kuchanganua tasfida kama mojawapo ya mkakati wa upole.

Habwe (1999) ameshugulikia mengi kuhusu mikakati ya upole. Kazi hii inatupa mwongozo katika kushugulikia dhana ya uso.

Brown na Levinson (1978, 1987) wanatusaidia kuelewa nadharia ya upole kwa undani kwani nadharia hii ilitokana na nadharia ya uso. Brown na Levinson wameshugulikia swala la uso na kuzianisha katika makundi mawili ambayo ni uso chanya na uso hasi.

### **1.7.1 Yaliyoandikwa kuhusu upole**

Upole ni namna ya kuonyesha adabu njema na kushughulikia mahitaji ya wanajamii wengine ya kupewa heshima. Ni dhana ambayo hufungamana na utamaduni kwa maana kuwa kinachotambulika kuwa na kukubalika kuwa upole katika jamii moja kinaweza kuwa kinyume cha upole katika jamii nyingine. Dhana ya upole ni pana na imefanyiwa utafiti kwa zaidi ya miongo mitatu. Uchunguzi kuhusu dhana ya upole ulipata umaarufu miaka ya sabini. Goffman (1967) alijadili upole katika muktadha wa jumla ya tabia. Mtazamo wa upole kama jumla ya tabia nzuri na mbaya, ni dhahiri katika mawasiliano japo kila jamii ina njia ya kipekee ya kuonyesha upole. Goffman alieleza kuwa upole ni utambuzi ambao mtu humwonyesha mwingine kupitia kutimiza au kuepukana na kaida au desturi fulani za mawasiliano.

Brown na Levinson (1978, 1987) wanaelezea upole kama namna ya kuokoa uso wa msikilizaji. Kulingana nao watu hutumia upole kama njia ya kuhifadhi matamano ya nyuso za wengine. Kwa mfano mtu akimwambia mwingine, “Hiyo nguo yako imekufaa sana, ulinunua wapi?”. Wakati anajua vizuri ukweli wa kauli hiyo ni kinyume. Kauli hii inaungwa mkono na Leech (1983) anaposema kuwa upole ni mkakati wa mawasiliano ambao watu hutumia kuanzisha na kuhifadhi mahusiano katika jamii.

Watts (2003:39) anasema kuwa upole ni hulka ya kiasili ya tabia njema. Ni uwezo wa kufurahisha kupitia matendo ya nje ya mtu husika. Aidha upole ni dhana ya kiakili na kijamii ambayo hukuzwa kupitia mahusiano yetu ya kijamii. Anabainisha kuwa watu hawazaliwi na upole bali wanajifunza kwa kutazama jinsi watu wengine wanavyotagusana katika jamii yao. Kauli hii inatiliwa nguvu na ukweli kuwa dhana ya upole ni tofauti katika jamii na tamaduni mbalimbali.

Upole ni dhihirisho la tamani la msemaji kupunguza vitisho kwa uso vinavyotekelezwa na vitendo fulani vinavyotishia uso wa mtu mwingine. Brown na Levinson (1978) wanasisitiza kwamba kila binadamu anapendelea kutambulika kwa kazi anayoifanya kwa hivyo ana nyuso mbili; uso hasi chanya. Nyuso hizi hupatikana kwa kila mtu ulimwenguni. Aidha wanasema kuwa nyuso hizi binadamu anaweza kuzihifadhi au kuzipoteza. Kwa kuzishugulikia nyuso hizi, waliibuka na mikakati ya upole ifuatayo: mkakati wa upole chanya, mkakati wa upole hasi na mkakati wa nje ya rekodi. Utafiti huu utafaidika sana kwani una jukumu kubwa katika kuchunguza upole.

### **1.8 Msingi wa nadharia**

Nadharia ya upole iliasisiwa na Brown na Levinson (1978, 1987) walitumia dhana ya uso ya Goffman (1967) kubuni nadharia ya upole. Nadharia ya upole ilipata umaarufu wake miaka ya sabini japo Goffman alikuwa ameshughulikia suala la upole hapo awali. Nadharia hii iliandikwa baada ya Goffman (1967) kuchapisha makala yake juu ya kazi za uso. Kulingana na Goffman (1967:5), uso ni thamani chanya ya kijamii ambayo mtu hujipa kulingana na mtazamo ambao wengine huchukulia kuwa ameegemea katika mtagusano fulani. Goffman (1967) anafafanua 'uso' kama kitu muhimu cha jamii ambacho mtu anadai kwa namna ambayo wengine wamechukulia amekipata wakati wa mtagusano fulani katika jamii. Aidha alikuwa amejadili upole katika muktadha wa nadharia ya jumla ya tabia, ambapo alieleza kuwa upole ni utambuzi ambao mtu humwonyesha mwingine kupitia kwa kutimiza au kuepuka kaida au desturi fulani za mazungumzo.

Goffman (1967) anasema kuwa kila mwanadamu ana nyuso za aina mbili, yaani nyuso za hadharani na nyuso za kibinafsi. Wanasosholojia walizungumzia nyuso hizi kama nyuso za watu kazini, nyumbani na kadhalika. Brown na Levinson (1978, 1987) wanasema kuwa kila binadamu anapendelea kutambulika kwa kazi anayoifanya kwa hivyo ana nyuso mbili, uso chanya na uso hasi. Nyuso hizi binadamu anaweza kuzipoteza au kuzihifadhi, zinategemea hisia. Kila binadamu anajali nyuso hizi kwa kuwa hataki kumvunjia mtu mwingine heshima. Uso si kitu cha kibinafsi kilichomo ndani au nje ya mwili wa mtu bali ni ishara inayopatikana katika mtiririko wa matukio yanayothibitishwa na maamuzi ya watu na nguvu inayojibainisha katika hali ya mitagusano katika jamii. Kwa hivyo uso ni ishara bayana katika jamii ambayo ni sharti itathaminiwe. Upole ni muhimu katika kuhifadhi uso chanya.

Brown na Levinson (1978) wasema kuwa dhana ya uso ni muhimu katika maingiliano ya binadamu. Nadharia hii ya upole iliibuka ili kuokoa uso kutokana na matendo ya kutishia uso. Upole ni namna ya kuokoa uso wa msikilizaji. Watu hutumia upole kama njia ya matamano ya nyuso za wengine na pia kutambua kuwa kuna vitendo vinavyotishia uso na kujaribu kuepukana navyo. Johnstone (2008) anasema kuwa wazungumzaji hawana budi 'kuokoa uso' wanapokabiliwa na tendo linalotishia uso wa msikilizaji. Kwa hivyo mzungumzaji hana budi kujua kwamba maneno yasiyokuwa na adabu na heshima daima hutishia uso. Mzungumzaji ni sharti ateue maneno yatakayofanikisha mawasiliano bila kupujua uso wa mwenzake na ajiepushe na maneno ya kutishia uso. Walitambua kwamba kuna vitisho vya uso. Vitisho hivyo husababishwa na ukosefu wa upole hasi na ukosefu wa upole chanya.

### **1.8.1 Vitendo vinavyotishia uso**

Kuna baadhi ya vitendo vinavyotishia uso. Brown na Levinson (1978) wamebainisha vitendo vinne ambavyo hutishia nyuso za wahusika katika mawasiliano ambavyo huweza kuathiri uso wa mzungumzaji au msikilizaji. Kwanza, vitendo vinavyotishia uso hasi wa msikilizaji ambavyo hutokea wakati ambapo msemaji anaingilia uso wa msikilizaji. Kwa mfano, kwa kumshauri, kutoa maonyo, kuamrisha au kutoa maagizo bila hiari ya msikilizaji. Pili, kuna vitendo ambavyo hutishia uso chanya wa msikilizaji.

Vitendo hivyo huweza kumtia aibu msikilizaji hivyo kuathiri uso chanya, kwa mfano kumdunisha mtu, kumtusi, au kuzungumzia mambo kuhusu maisha yake kwa namna isiyokubalika. Tatu, vitendo ambavyo hutishia uso hasi wa mzungumzaji kama vile kukubali pendekezo fulani, kukubali kusamehe na kuahidi jambo fulani bila kupenda au kukubali shukrani kutoka kwa msikilizaji. Nne, vitendo vinavyotishia uso chanya wa msemaji. Kwa mfano, kukiri makosa na kujidunisha mbele ya msikilizaji, kukubali pongezi na kumwomba msamaha. Mikakati ya upole hasi na upole chanya ilibuniwa katika kujaribu kuokoa uso kutokana vitishio vya uso ili kudumisha mitagusano. Katika kukabiliana na vitendo vinavyotishia uso, Brown na Levinson (1978, 1987) walibuni mikakati mitano ya kuokoa nyuso kama ifuatavyo:

1) Mkakati chanya wa upole

Mkakati huu unahusu kuonyesha heshima kwa msikilizaji na kuashiria uhusiano baina ya msemaji na msikilizaji. Mkakati huu hutilia mkazo uhusiano baina ya msemaji na msikilizaji hivyo kumweka msemaji katika hatari ya kuonyesha uhusiano baina yao.

2) Mkakati hasi wa upole.

Mkakati huu pia unashughulikia kupunguza ulazimishaji wa taarifa kutoka kwa msikilizaji.

3) Mkakati kuwa kwenyerekodi.

Mkakati huu hautilii maanani mahitaji yoyote ya uso lakini unakubalika katika hali ya dharura. Katika mkakati huu msemaji husema taarifa husika jinsi ilivyo.

4) Mkakati wa kuwa nje ya rekodi.

Pia huu mkakati unahusu kuwasilisha habari kwa njia isiyo ya moja kwa moja au kwa njia isiyo ya kimapumbo. Katika mkakati huu, ni vigumu kuhusisha usemi husika na lengo moja tu, hivyo kumwacha msikilizaji kufasiri usemi husika jinsi atakavyo. Huzingatia usalama lakini msemaji hukabiliwa na hatari ya msikilizaji kuifasiri habari visivyo.

5) Mkakati wa kutowasilisha ujumbe kabisa.

Mkakati huu ndio una kiwango kikubwa cha upole lakini msemaji anapoutumia huwa hatimizi lengo lake.

### **1.8.2 Uso hasi**

Uso hasi ni uso ambao haupendi kuingililiwa na wengine kwani kila mwanadamu hudai uhuru wake. Mwanadamu yeyote huwa hataki kuingiliwa, kuombwa, kutembelewa bila hiari, kupewa habari mbaya kuhusu yeye mwenyewe, watoto wake au jambo lolote kuhusu maisha yake. Uso hasi unaweza kupotezwa ikiwa mtu anaweza kujiingiza katika mambo ya mtu mwingine bila idhini au hiari yake. Hii inawezekana kwa kuombwa kitu chake ihali hataki kuombwa, kumwambia akufanyie jambo fulani ilhali hataki kufanya, au kujikaribisha kwa mtu ambaye hajisikii kukukaribisha. Uso huu unataka kumwachia mtu uhuru wake bila kuumiza hisia zake. Katika uso huu, mtu anataka atende vitu vyake kivyake. Goffman (1967:9) anasema kuwa kutunza uso humfanya mtu kuhisi vizuri. Kwa mfano katika hii sentensi: “Njoo uninunulie chai”, au “Lete gari lako tulitumie”. Sentensi hizi huonyesha kuingilia mtu kwa kuumumiza hisia zake.

Matarajio ya uso hasi ni kumuacha mtu kuwa na uhuru bila kuumiza hisia zake. Uso huu hukumbwa na tishio wakati mtu hatarajii kukwepa tendo la uhuru wa msikilizaji wake katika mawasiliano. Mwanadamu yeyote huwa hataki kunyimwa haki ya kujiamulia mambo yake. Vitendo vya kutishia uso wa msikilizaji humlazimu mzungumzaji kubuni mbinu mbalimbali za upole ili kuokoa uso wa msikilizaji. Jambo hili huboresha mahusiano baina ya wahusika na vile vile kuhakikisha mawasiliano yameendelea bila kuvunjika. Kwa hivyo uso hasi ni tamanio la kutaka kujiwekea mipaka ya uhuru wa kutoingiliwa kwani ni uso unaohitaji uhuru.

### **1.8.3 Uso chanya**

Uso chanya ni uso wa binadamu unaopenda kutambuliwa, kusifiwa, kuheshimiwa na kujumlishwa katika shuguli za kijamii. Haupendi kutengwa wala kuhimiliwa. Uso huu hudhuriwa pale ambapo mzunguzaji au msikilizaji hajali yule anayewasiliana naye. Kila mwanadamu anapenda kutambulika, kushirikishwa katika shughuli za kijamii, kusifiwa na kutobaguliwa. Kwa mfano: Wanawake wanapoulizana, “Nguo yako nzuri kweli, ulishonewa wapi?”. Wakati mwingine swali kama hili halifungamani na ukweli, ni kwa lengo tu la kutaka kuhifadhi uso. Uso chanya ni tamanio la kutaka kukubalika na wanajamii wengine. Uso huu unapokosa kusifiwa au kutambuliwa, unaweza kudhuriwa.

Kwa hivyo msemaji ana jukumu la kuteua mikakati ya kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kupunguza vitisho kwa uso wa msikilizaji. Brown na Levinson (1987) wanaeleza kwamba “uso” unafaa kutiliwa maanani kila wakati katika mazungumzo kwa sababu unaweza kupotezwa, kuhifadhiwa au hata kuendelezwa.

#### **1.8.4 Mkakati wa upole hasi**

Huu ni mkakati ambao ulibuniwa na Brown na Levinson (1987:29) ili kuhifadhi uso hasi. Uso hasi ni kule kuingilia uhuru wa mtu. Brown na Levinson (1987:29) wanaeleza kuwa mkakati hasi wa upole ni mahususi na hulenga katika kupunguza ulazimishaji wa kauli fulani inayotishia uso wa msikilizaji na hautumiki kwa namna huria katika mawasiliano kama ilivyo kwa mkakati chanya wa upole. Huu ni mkakati unaotumika wakati msemaji anataka jambo au kitu fulani kutoka mtu msikilizaji lakini anataka kuhifadhi haki yake ya kukataa, kwa sababu anafahamu kuwa huenda ikawa msikilizaji wake hataki kuingiliwa labda kwa kuombwa au kuulizwa jambo fulani.

Mkakati hasi wa upole husizitiza tofauti zilizopo baina ya msemaji na msikilizaji. Hii ni kwa sababu wakati mwingine msemaji anaweza kulazimisha matarajio yake kwa msikilizaji na kwa hivyo kuna uwezekano mkubwa wa kufedheshwa. Kwa sababu msemaji anataka kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji, analazimika kutumia mkakati hasi wa upole kwa kutumia mbinu mbalimbali. Mbinu hizo ni kama vile maswali na vidokezo, kwa mfano, “Nashangaa kamaungeweza kunisindikiza nyumbani?”. “Inawezekana uniazime kalamu yako?”. Kutumia vitangulizi, kwa mfano, “Hebu ninunulie hii chakula, hali yangu si nzuri, au “Samahani niruhusu nikuingilie mwanangu, unaona vipi kutomuoa yule mke?” Vitangulizi hutumika kama njia ya kumtayarisha msikilizaji kwa jambo unalotaka kusema. Mbinu zingine ni kama vile, kunominisha, kwa mfano “kutofanya bidii katika masomo kutakufanya ufeli mtiani yako” badala ya kusema “ulianguka kwa sababu hukufanya bidii”. Kutaja kanuni ya jumla kwa mfano, mwalimu anaweza kuwambia wanafunzi “Hakuna kutoka nje leo” badala ya kumwambia mwanafunzi mmoja aliyetoka nje asitoke ili kuhifadhi uso hasi wa mwanafunzi huyo. Kuwa bila rujua, kwa mfano, “Najua huna namna ya kunisaidia lakini kusema ukweli, leo nahitaji msaada” ili kuhifadhi uso wa msikilizaji.



Mbinu zingine zaweza kuwa zenye mzunguko lakini matarajio ya mzungumzaji ni kuwa jibu lipatikane. Wakati mwingine mzungumzaji analazimika kutumia njia ya udanganyifu, kusudi aweze kuepukana na kudhuru uso wa msikilizaji, yaani hataki kumwambia ukweli kwa njia ya moja kwa moja ikiwa jambo halimpendezi. Kwa mfano, msemaji anaweza kusema, “Waonaje viatu vyangu, je, vimenikaa vizuri?”. Japo viatu havijamkaa vizuri inambidi kukubaliana naye kwa sababu ya kutotaka kumpujua uso, badala yake atamsifia na hata kutaka kujua ni duka lipi au ni wapi alinunua hivyo viatu, badala ya kumuaibisha. Ili kuhifadhi uso hasi, msemaji anatumia mkakati hasi wa upole.

### **1.8.5 Mkakati wa upole chanya**

Huu ni mkakati wa kumtambua mtu, kumshirikisha katika shughuli za kijamii, kumsifu, kumheshimu au hata kumshukuru ili kuhifadhi hadhi ya mzungumzaji katika jamii. Brown na Levinson (1987:101) wanaeleza kuwa mkakati wa upole chanya huelekezwa kwa uso chanya wa msikilizaji na tamani lake kuwa mahitaji yake yatatiliwa maanani. Mkakati huu wa upole chanya hutumika kuashiria kuwa msemaji na msikilizaji wote wana lengo moja au msimamo sawa. Aidha Brown na Levinson (1987:106) wanaelezea kuwa mkakati huu ni hulka ya kawaida miongoni mwa marafiki na watu wengine ambao wana uhusiano wa karibu. Mkakati huu hujaribu kuinga uso au kuokoa uso chanya wa msikilizaji kwa kumfanya kuhisi vizuri kuhusu matarajio yake.

Hali ya kuwepo kwa tishio la uso wa mtu ni tendo linalohitaji kuingwa kwa kutumia maneno ya upole ili kuafikia lengo la mawasiliano. Mzungumzaji huwa na jukumu kubwa la kuteua maneno ya kumheshimu msikilizaji. Wakati mwingine maneno makali na yenye uchukivu na ukosefu wa heshima hutishia uso, kwa hivyo ni muhimu msemaji kufahamu kuwa uchaguzi wa maneno ni wa manufaa kwani unafanya lengo la mawasiliano kufanikishwa. Kwa mfano,

- i) “Hongera kwa kazi nzuri uliyoifanya, hata ingawa kuna shida kidogo”.
- ii) “Chakula hiki umepika leo ni kitamu sana, naomba chumvi kidogo niongezee”.

Katika sentensi ya kwanza msemaji anataka kumjulisha msikilizaji kuwa kazi yenyewe ina kasoro fulani lakini hataki kumwambia moja kwa moja. Katika sentensi ya pili

mzungumzaji anataka kumjulisha mwenzake kwamba chakula alichokipika kina upungufu fulani, lakini hataki kumwambia kwa njia ya moja kwa moja ila anaanza kwa kumsifu kuhusu mapishi yake. Katika hali hii mzungumzaji ametumia mkakati wa upole ili kuokoa uso. Kimsingi mzungumzaji huepukana na kumkera msikilizaji wake ili kuokoa uso.

Mkakati chanya wa upole hutekelezwa kwa kuepuka kutokubaliana na msikilizaji kama njia ya kuokoa uso chanya. Kwa mfano, iwapo msemaji atakuuliza kama utaenda kazini na unajua hautaenda, usimwambie kuwa hauwezi bali kubali kisha uongeze kauli fulani ambayo kwayo itakuruhusu kutotekeleza ulioahidi ikiwa ataelewa. Kwa mfano, “Utaenda kazini kesho asubuhi?” Unamjibu kuwa ndio lakini itategemea vile nitakavyoamka kesho. Ikiwa ataelewa muktadha, basi atajua kuwa hautaenda kazini. Kutumia ucheshi, kwa mfano, Kazi zingine za ziada zinahitajika kufanywa leo. “Naona leo umemaliza kazi yako ya ziada!” Vile vile kuna njia ya kuahidi, kutoa sababu za kitendo fulani na kutafuta makubaliano. Brown na Levinson (1987) wanaeleza kuwa msemaji anaweza kuhifadhi uso chanya wa msikilizaji kwa kutafuta makubaliano naye. Hivyo msemaji husema tu mambo ambayo anatarajia msikilizaji akubaliane nayo, yaani yale yanayopunguza taharuki. Kwa mfano, “Nakubaliana nawe kuwa leo kutanyesha”. Huu ni mkakati ambao msemaji hutumia maneno kwa makini ya hali ya juu kwa kuzingatia anayezungumzia.

### **1.8.6 Mahitaji ya uso**

Yule (1996:61) anarejelea dhana ya ‘uso’ kama ‘mahitaji ya uso’ na kusema kuwa watu hufanya mambo wakiwa na matarajio kuwa mitazamo ya umma kuwahusu itaheshimiwa. Kwa kawaida kila mtu atatarajiwa kuheshimu mahitaji ya uso wa mwingine. Kwa hivyo naye anaunga mkono hoja kuwa kuna njia nyingi ya kutekeleza vitendo vya kuokoa uso. Aidha haistabili kupujua mtu uso kwani ni njia mojawapo ya kukosa heshima na adhabu. Hata hivyo ni vyema kila mtu kuelewa kwamba kila aina ya uso ina mahitaji yake ambayo ni tofauti na mahitaji hayo ni ya kipekee.

### **1.8.7 Mikakati ya kuheshimu uso**

Brown na Levinson (1978:61) wanasema kuwa kila mwanadamu katika jamii ana nyuso mbili, mbazo angependa zihimiliwe na kutambulika kwa kazi mbalimbali. Kila mwanadamu anazijali nyuso hizi kwa kuwa hataki kumvunjia mtu mwingine heshima. Aidha kujua sarufi ya lugha tu haitoshi kwa sababu lazima hiyo sarufi ifungamane na upole. Kuna mambo mawili ambayo hufanyika kwa uso ambayo ni kuheshimiwa au kudhuriwa.

Katika mawasiliano, heshima inawahuisisha mzungumzaji au msikilizaji kwa sababu wote wawili wanashirikishwa katika mawasiliano. Hata hivyo kuna baadhi ya mazungumzo ambayo yanaweza kuvuruga uso chanya kutokana na msemaji kutojali hisia. Brown na Levinson (1978: 62) wanadai kuwa mazungumzo yanahusiana zaidi na kuchunguza matarajio ya upole yanayolenga uso kwa ujumbe unatolewa. Kutokana na madai haya dhana ya upole hasi, upole chanya na mkakati wa rekodi zilijitokeza kwa mujibu wa kuokoa uso.

### **1.8.8 Upole chanya**

Huu ni mkakati ambao unahusisha watu wawili ambao wana uhusiano wa kupunguza vitendo vinavyotishia uso chanya. Mkakati chanya wa upole hutumika pale ambapo mzungumzaji anatumia mbinu ambazo zaweza kumpatia msikilizaji uhuru katika mazungumzo. Mbinu hizi ni kama vile kupongeza, kusifu au ucheshi kwa sababu ya kupunguza tishio la uso. Kwa upande mwingine mzungumzaji anaweza kuzua maneno ya upole kwa kutumia ahadi au mzaha katika mazungumzo. Kwa mfano msemaji anaposema, “Ukimaliza kufanya hii kazi nitakupeleka matembezini”, “Ukipata alama mia nne na zaidi nitakununulia baiskeli”. Kwa kutumia mzaha, “Ahaah mrembo, leo umerembeka kweli? Unaonekana kama bi harusi!”. Huu ni mkakati pia unaohusisha watu katika shughuli fulani. Kwa mfano, “Iwapo tutalima shamba hili vizuri wakati huu tutapata mavuno mazuri”.

Mambo mengine ambayo mkakati huu hutekeleza ni kama vile, kumpa mtu matumaini. Kwa mfano, “Mwaka ujao nikipata pesa nitakununulia gari”. Vile vile hutumika

kuzidisha au kutia chumvi kwa faida ya msikilizaji. Kwa mfano, “Ahaa! Leo u mrembo sana! Kwani unaenda arusini?”. Brown na Levinson (1987:106) wanaeleza kuwa upole chanya ni hulka ya kawaida miongoni mwa marafiki na watu wengine ambao wana uhusiano wa karibu.

### **1.8.9 Upole hasi**

Brown na Levinson (1987:129) wanasema kuwa upole hasi ni mahususi na hulenga kupunguza ulazimishaji wa kauli fulani inayotishia uso wa msikilizaji. Kama vile walivyopendekeza hapo mbeleni, ni lazima kutafuta mbinu ya kuokoa uso hasi ili kutodhuru watu wengine. Kuna uwezekano wa kudhuru hisia za mtu mwingine ikiwa njia ya kuingiliana haina utaratibu maalum.

Uso hasi hautaki kuingiliwa, yaani unahitaji uhuru wake. Kuna uwezekano wa kudhuriwa ikiwa mtu anaweza kuomba kitu kutoka kwa mwenzake bila kujali uso hasi wa hadhira na huenda uso huo ukakosa amani. Njia mwafaka ya kutodhuru huu uso ni kwa kutumia upole hasi. Njia zifuatazo hutumika, kutumia njia za mzunguko au maswali. Kwa mfano, “Huenda tukasafiri Kisumu wakati wowote unaweza kuniletea hizo nguo?”. Kutokuwa dhahiri, kwa mfano, mume anamuuliza mke wake, “Je umeona mahali niliweka pesa zangu?”

### **1.8.10 Mkakati wa kuwa kwenye rekodi**

Mkakati huu hutumiwa na wazungumzaji ambao wana uhusiano wa karibu sana. Malengo ya huu mkakati si wa kuhifadhi uso wa msikilizaji. Kuhusu huu mkakati, mzungumzaji mara nyingi anasisitiza ujumbe anaotaka kuwasilisha bila kujali mahitaji ya uso au vitishio vya uso. Mkakati huu hutumiwa na watu ambao wanaweza kushirikiana kuhusu mambo fulani. Unahusu watu wa karibu sana kama vile watu wafamilia au marafiki wa karibu sana. Katika mkakati huu, msemaji husema jambo au habari moja kwa moja kwa hadhira, hali ambayo inaweza kuathiri uso hasi. Hata hivyo ni mkakati unaotumika kusema ukweli moja kwa moja japo kwa njia ya upole. kwa mfano, “Chunga, kuna mbwa mkali sana hapo”. Sentensi hii huonyesha jambo la dharura. Mkakati huu pia unaweza kutumika kutoa ahadi. Kwa mfano, “Nitakununulia

kitabu kesho”. Hapa inambidi msemaji kutumia lugha ya upole kwa sababu msikilizaji ndiye mfaidi. Mkakati huu hutumika vile vile pale ambapo kitendo ni cha kumfaidi msikilizaji. Kwa mfano, “Lete hivyo viazi nipike”.

Brown na Levinson (1987:95), wanaeleza kuwa mzungumzaji anapotaka kufanya kitendo kinachotishia uso kwa ufanisi zaidi ili kutosheleza uso wa msikilizaji kwa kiwango chochote kile, anatumia huu mkakati wa kuwa kwenye rekodi. Haya yanatokana na kuwa huu mkakati lengo lake si kushughulikia mahitaji yoyote ya uso kati ya msemaji na msikilizaji. Brown na Levinson (1987:69) wanasema kuwa mkakati huu hufuata kaida za ushirikiano za Grice (1975). Grice (1971) alijadili suala la lugha na mawasiliano na kujaribu kutathmini mchango wa msemaji katika diskosi na msikilizaji wake. Alidai kwamba kila mtagusano lazima kuwepo na ushirikiano unaosimamiwa na utaratibu wa kiuwiano ili kuhakikisha kwamba mazungumzo baina ya watu hayavunjiki. Alidai kwamba utaratibu huu una kanuni nne ambazo ni za ushirikiano. Kanuni za ushirikiano za Grice (1975) ni nne: kwanza kuna kanuni ya idadi ambayo inahimiza mtu kutoa mchango wake katika mazungumzo inavyostahili au inavyohitajika. Mchango wa mtu katika mazungumzo uwe ni ule wa mkondo wa mazungumzo.

Pili ni Kanuni ya ubora ambayo husema kuwa mchango ambao mtuanaotoa katika mazungumzo uwe wa ukweli. Mtu asiseme jambo ambalo ni la uongo au asiloweza kuthibitisha. Tatu kuna kanuni ya kiwango: kanuni hii husema kuwa mtu atoe mchango wake katika mazungumzo kwa kutoa habari ya kutosha. Asitoe habari zaidi ya kiwango kinachostahili. Kanuni ya mwisho ni kanuni ya ufaafu: kanuni hii husema kuwa mtu asipotoke kutoka kwa mazungumzo. Msemaji anafaa kujiepusha na kauli tata ambazo huweza kuibua fasiri mbalimbali. Msemaji anafaa kueleza kauli zake kwa uwazi. Kauli hizi hazijali mahitaji ya uso, lakini bado zinadumisha upole. “Ndugu yangu, kitabu chako kimeanguka .....” kauli hii huonyesha kutokuwa na haja ya kujali uso lakini bado inadumisha upole.

### **1.8.11 Mkakati wa kuwa nje ya rekodi**

Huu ni mkakati wa kusema mambo kimapumbo ili yasiathiri uso hasi au uso chanya. Mkakati huu wa upole sio wa moja kwa moja kwani mzungumzaji hueleza kitu au jambo kwa njia ya mzunguko. Msemaji huteua maneno yasiyo ya moja kwa moja na kuyatumia kupitisha ujumbe. Aidha msemaji halazimishi matarajio yake kwa msikilizaji bali anadokeza tu jambo fulani na kumwacha msikilizaji kuufasiri huo ujumbe atakavyo. Brown na Levinson (1987:211) wanasema kuwa si rahisi kuhusisha lengo moja wazi katika usemi husika. Utata huu unaafikiwa kwa kuvunja kanuni ya ushirikiano ya Grice (1975) na hivyo kumwacha msikilizaji kufasiri maana atakavyo. Kanuni za Grice ni za jumla ya ushirikiano. Kanuni hizi husheheni vitengo vinne ambavyo ni idadi, ukweli, uhusiano na namna. Hizi kanuni hufafanua namna mawasiliano huafikiwa katika hali za kawaida za kijamii. Aidha hutoa maelekezo kuhusu matumizi ya lugha katika mazungumzo. Grice anaelezea kuwa kanuni ya ushirikiano inahusu wasemaji na wasikilizaji. Msemaji na msikilizaji wanaozingatia kanuni ya ushirikiano huhakikisha kuwa jambo wanalozungumzia linaendeleza mawasiliano. Kuvunja kanuni za ushirikiano huweza kukubalika kama ishara ya lengo mahususi la msemaji.

Mkakati wa nje ya rekodi si dhahiri kwa kuwa msikilizaji anaweza kufasiri ujumbe husika visivyo na kwa hivyo kumfanya msemaji kutoafikia lengo lake. Kwa mfano msemaji anaweza kusema hivi akitaka apewe chai, “Tangu jana sijakunywa chai”. Katika sentensi hii msemaji hasemi mahitaji yake kwa njia ya moja kwa moja. Msemaji anaweza kukosa kuafikia lengo lake kwa sababu msikilizaji anaweza kumwambia, “pole kwa kutokunywa chai”. Mkakati huu ni salama kutumiwa katika juhudi za kuokoa nyuso za wazungumzaji licha ya kuwa inamchukua msikilizaji muda mrefu kufasiri ujumbe wa msemaji kulingana na matarajio yake. Mkakati huu wa kuheshimu uso ni mbinu inayotumiwa kupitia kwa matumizi ya upole.

### **1.9 Njia za utafiti**

Kazi hii ni ya utafiti fafanuzi kwa kuwa utafiti fafanuzi ni utafiti unaochunguza data hali ilivyo kwa wakati fulani na kuifafanua lugha na kuripoti jinsi ilivyo.

### **1.9.1 Mbinu za ukusanyaji data**

Tulitumia data za nyimbo za harusi za Kiswahili na nyimbo za harusi za Ekegusii na data za maktabani ambazo zimeandikiwa kuhusu tasfida. Tulipata data ya uchunguzi kwa kusikiliza na kurekodi nyimbo hizi kutoka kwa wazungumzaji asilia wa lugha ya Ekegusii. Tulichagua nyimbo hizi kwa sababu lugha ambayo inatumika katika nyimbo ina matumizi mengi ya lugha ya adabu. Aidha ni lugha ambayo si ya moja kwa moja na hutumika kukuza na kuendeleza maadili katika jamii.

### **1.9.2 Mbinu za uchanganuzi na uwasilishaji wa data**

Tulichunguza data yetu baada ya kunakili kauli zilizoendeleza upole. Kauli hizi tulizifafanua kwa misingi upole ya nadharia ya upole iliyoasisiwa na Brown na Levinson (1978) ili kuthibitisha kama kuna uwiano wa tasfida za lugha za Kiswahili na Ekegusii na kuiwasilisha kwa njia ya maelezo.

## **1.10 Hitimisho**

Katika sura hii tumeweka msingi wa utafiti wetu kwa kueleza tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada hii, upeo na mipaka ya utafiti wetu, misingi ya nadharia, uteuzi wa sampuli, njia za utafiti, ukusanyaji wa data, na uwasilishaji wa data. Pia tuliangazia suala la tasfida kama lilivyoshugulikiwa na watafiti wengine, na mchango wao katika uchunguzi wetu. Aidha tumefafanua nadharia ya upole kama ilivyopendekezwa na Brown na Levinson (1978, 1987) ili kutuongoza katika uchunguzi wetu hasa jinsi suala la upole linavyoshugulikiwa katika matumizi ya tasfida za Kiswahili na Ekegusii. Aidha tumeeleza mikakati ya upole kama vile mkakati chanya wa upole, mkakati hasi wa upole, mkakati wa kuwa kwenye rekodi na mkakati wanje ya rekodi. Aidha tumeelezea historia fupi kuhusu lugha za Kiswahili na Ekegusii kwa tutarejelea tasfida za lugha hizi. Tumeeleza mambo ya kimsingi kuhusu uchunguzi wetu mbayo yatatuongoza katika sura zitakazofuata ili kuendeleza uchunguzi huu.

## SURA YA PILI

### HALI ZINAZOZUA MATUMIZI YA TAFIDA

#### 2.1 Utangulizi

Katika sura ya kwanza, tumejenga msingi wa kazi yetu kwa kuwa inalenga tasfida za Kiswahili na Ekegusii kama mkakati wa upole. Katika sura hii tutachunguza hali zinazozua matumizi ya tasfida za Kiswahili na Ekegusii. Katika mawasiliano ya kila siku mzungumzaji anapaswa kuteua maneno ya tasfida kulingana na hali, na uhusiano wa kijamii. Uteuzi huu huonyesha upole kwa msikilizaji. Hali mbalimbali katika jamii huzua matumizi ya tasfida ili kuokoa nyuso. Ili kuelewa kikamilifu hali hizi, ni muhimu kuelewa dhana ya tasfida, historia pamoja na aina za tasfida. Harry (1954) anasema kuwa lugha huashiria mfumo wa jamii husika na kwa hivyo kuna uhusiano baina ya lugha na jamii ambapo lugha hiyo hutumika. Tasfida hutokana na shughuli za kijamii za kila siku na aghalabu hutumika kuonyesha upole. Maoni haya yanasawiana na Katamba (1985) anayeeleza kwamba tasfida ni neno ambalo hutumika kufafanulia lugha, mawazo, na dhana ambazo hupunguza uchukivu wa utamaduni miongoni mwa wanajamii. Uamilifu wa tasfida ni kudumisha na kufanikisha mawasiliano. Kwa mfano, kujifungua, na kujisaidia ni maneno yanadhihirika katika Kiswahili na Ekegusii ili kukoa uso. Tasfida, uso na upole ni mambo ambayo yanahusiana kwa lengo la kufanikisha mawasiliano. Mawasiliano ya watu huelekezwa na kutawaliwa na vigezo vya kitamaduni, au miktadha ya kitamaduni. Katika hali hii, mawasiliano yanahusu tabia za watu katika uzungumzi kwa mujibu wa utamaduni uliopo. Wazungumzaji hulazimika kutumia maneno ya upole ili kuhifadhi nyuso za wasikilizaji wao. Pasina upole patakuwa na mitafaruku na migongano miongoni mwa wanajamii.

#### 2.2 Dhana ya tasfida

Allan na Burridge (1991) wanasema kuwa tasfida ni tafsiri ya neno '*euphemism*' ambalo lilitokana na neno la kigiriki '*eu*' ambalo humaanisha nzuri na '*pheme*' ambalo humaanisha kuzungumza. Tasfida kwa tafsiri ya '*eupheme*' humaanisha kuzungumza kwa maneno mazuri na kwa usemi usiodhuru. Gatambuki (2009) akirejelea mawazo ya Enright (1985) na Allan na Burridge (1991) anadai kuwa tasfida ni kutumia maneno mazuri, matamu, yanayopendeza, yaliyotiwa nakshi na ya kuvutia na kutosema maneno



kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja ili kuepuka kudhuru uso wa watu wengine katika mawailiano. Kwa hivyo tasfida ni mbinu ya lugha ambayo hutumika kuficha maneno ya aibu yasiyosemwa hadharani ili kukinga uso. Tasfida inahusishwa moja kwa moja na mambo ya kijamii ya heshima na tabia za upole zinazohitajika katika mawasiliano.

Brown na Levinson (1983:5) wanaeleza kwamba muktadha huathiri matumizi na uteuzi wa msamiati katika kujenga maana kwa lengo la kukuza na kuendeleza mawasiliano. Utamaduni hujengwa na kudumishwa na watu wa jamii moja wenye utamaduni mmoja. Wanajamii wanapaswa kuwa na lugha ya upole kimazungumzo au kimaandishi. Trudgil (2002:58) anaeleza kuwa mazungumzo hutofautiana na muktadha wa kijamii ambapo mzungumzaji hujipata. Hii ni kwa sababu kila lugha ina ruwaza fulani, utamaduni na njia za kuteua maneno yanayotumika katika muktadha mbalimbali. Kwa mfano katika Kiswahili, neno '*makalio*' ni neno la upole linalotumika badala ya neno '*matako*'. Lugha zinazopatikana ulimwenguni zina njia tofauti za kuonyesha upole kwa kuwa tasfida hupatikana katika lugha zote ulimwenguni. Kuna baadhi ya maneno katika lugha ya Ekegusii ambayo hutumika mahala popote na wakati wowote pasina kuvuruga mahusiano wala kuleta uchukivu miongoni mwa wanajamii licha ya kuonekana kama ni ya aibu. Kwa hivyo ni dhahiri kwamba si maneno yote katika kila lugha yanaweza kutafutiwa tasfida. Kwa sababu hii huwa hayahitaji matumizi ya tasfida.

### **2.3 Kanuni za matumizi ya tasfida**

Gatambuki (2009) akimrejelea Zisheng (2005) aeleza kuwa kila aina ya tasfida hutumiwa kulingana na kanuni zifuatazo:

- (1) Kanuni ya urefu
- (2) Kanuni ya uhusiano
- (3) Kanuni ya kusitiri uso
- (4) Kanuni ya starehe

#### **2.3.1 Kanuni ya urefu**

Kanuni hii hurejelea hali ambapo maneno ya miiko yametumika kwa mda mrefu na huelekea kupoteza umuhimu wake. Kwa sababu hii, mtu huhusisha maelezo ya tasfida

moja kwa moja na kile kinachorejelewa na tasfida hiyo. Kutokana na hali hii, tasfida mpya huundwa. Athari ya tasfida kwa muundo wa lugha huwa na uwiano wa moja kwa moja wa urefu katika ishara ya isimu na kirejelewa kama anavyodai Gatambuki (2009).

### 2.3.2 Kanuni ya kukinga uso

Kanuni hii hueleza kwamba dhana ya kukinga uso huendelezwa na wazo kuwa, kwa kutumia tasfida mtu huweza kujenga uso chanya katika mawasiliano na uwezo wa kujikinga na kuinua hadhi yake katika fikira za wasikilizaji. Grice (1975) anasema kuwa kanuni hii huwiana na mawazo ya nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1978, 1987) ambayo tunatumia katika uchunguzi wetu. Uchunguzi wetu unahusishwa na kanuni ya kukinga uso ambapo tasfida hutumika kuendeleza upole na kukinga nyuso za kijamii.

### 2.4 Historia na maendeleo kuhusu tasfida

Matumizi ya tasfida miongoni mwa wanajamii si swala geni kwa sababu wanajamii wamekuwa wakitumia maneno yaheshima. Inaarifiwa kwamba wanahistoria wa Kigiriki akiwemo Plutarch katika karne ya 1 anasema kuwa Waathenia wakongwe walikuwa wanafunika mambo mabaya kwa kutumia maneno ya upole kuyafanya yapendeze yanapotumika hadharani. Kwa mfano walitumia neno '*wenzi*' badala ya neno '*malaya*' '*mchango*' badala ya neno '*ushuru*' na '*jumba*' badala ya neno '*jela*', Fromkin, Rodman na Hymes (2003). Pia makala yamechapishwa kuhusu tasfida ambazo hushugulikia mada kama vile tasfida za watoto na tasfida za uanahabari, na kuonyesha jinsi zinavyotuimika tofauti kuhusiana na jamii pana (Enright 1985). Kwa hivyo kunaaina mbalimbali za tasfida kama vile, tasfida chanya na hasi, tasfida ng'amuzi na tasfida ng'amuzi bwete, tasfida za desturi na tasfida zisizo za desturi, tasfida misimu na tasfida endezezi, tasfida za kikazi na tasfida za kitaaluma, na tasfida za anatomia. Kwa kuwa tasfida hizi zitatupa mwongozo wa kazi ya baadaye, tutafafanua baadhi ya aina hizi za tasfida kama ifuatavyo:

#### 2.4.1 Tasfida chanya na hasi

Rowson (1981), aliainisha tasfida katika kategoria chanya na na hasi. Alieleza kuwa tasfida chanya hutiwa chuku na kuonekana muhimu sana kuliko vile zilivyo. Rowson (1981) anadai kuwa Waingereza na Wamarekani hupendelea tasfida ambazo zimetiwa chuku hasa kutafsidi kitu ambacho hakipendezi na kinadhuru. Katika tasfida zinazohusu watu wanaofanya kazi ndogo ndogo na duni, tasfida chanya hunuia kuinua hadhi ya kazi hizo ili kutopujua uso wa wanaofanya kazi hizo au kufanya kazi zenyewe zionekane nzuri. Maneno ya tasfida chanya hutiwa nakshi katika matumizi ya misamiati ya biashara, uanajeshi na kisiasa. Katika Ekegusii kwa mfano, mganga huitwa '*omonyagitari*' lenye maana daktari badala ya neno lenyewe '*omoriori*', bawabu huitwa '*omoruoti*' lenye maana mfalme nayaya huitwa '*omoiseke*' lenye maana msichana. Maneno hayo hutumika kama tasfida zinazokinga uso kutokana na kazi wanazozifanya. Tasfida hasi pia huitwa tasfida za kiutamaduni kwa sababu ni kongwe sana na zina uhusiano wa karibu na miiko. Kwa mfano katika Ekegusii; '*omisire*' yenye maana machweo na '*omosome*' yenye maana giza ni tasfida zinazorejelea kifo. Licha ya kuwa tasfida hizi ni hasi, zinatumika kuhifadhi uso wa msikilizaji kwa sababu zina upole kiasi kuliko maneno yenyewe ya miiko. Tasfida hizi pia hutumika kudumisha mawasiliano na kusitiri uso kwa kuondoa uwezo wa maneno ya miiko.

#### 2.4.2 Tasfida za desturi na zisizo za desturi

Levinson (2002), anadai kuwa kipragmatiki tasfida huweza kuanishwa kama tasfida za desturi na tasfida zisizokuwa za desturi. Tasfida za desturi nizile ambazoumaanisho wake tayari umekita mizizi. Mtindo wa kuandika na maana ya kipragmatiki tayari imekita mizizi ya matumizi na huwa dhana ya maana ndiyo imeachwa nje. Kwa kuwa umaanisho wake tayari umepatamizizi, sitiari ya tasfida hizi yaweza kutambulika na maana ya kipragmatiki inayokusudiwa kwa urahisi. Kwa mfano; Katika lugha ya Ekegusii, '*okonyekire*' yenye maana amezaidika ni tasfida inayomaanisha kujifungua. '*nare nabageni*' yenye maana ana wageni ni tasfida inayomaanisha hedhi. Aidha katika Ekegusii kuna majina ya wanyama au wadudu ambao majina yao hayatajwi moja kwa moja nyakati fulani. Kwa mfano '*engendanse*' yenye maana inayotambaa hutumiwa kurejelea nyoka badala ya neno la kawaida. '*Ebiromi*' yenye maana vinavyouma ni

tasfida inayotumika kurejelea siafu. Hizi tasfida hutumika kuashiria nyoka na siafu wakati wa usiku. Aidha kuna tasfida zinazorejelea wakati. Kwa mfano katika Ekegusii, '*amaiso abakungu*' yenye maana macho ya wananawake ni tasfida inayotumika kurejelea giza badala ya neno lenyewe '*egesunte*' lenye maana giza. Pia kuna tasfida kama '*gosoka kabere*' yenye maana kutoka mara mbili ambayo ni tasfida inayotumika kumrejelea mchawi. Maneno nyoka, siafu, giza na mchawi hutajwa vile yalivyo katika Kiswahili.

Kwa upande mwingine tasfida zisizo za desturi huwa hazijakomaa na umaanisho wake huwa unategemea muktadha. Kwa hivyo bila kuwa na msingi kamili wa ufahamu wa miktadha, inaweza kuwa ni vigumu kuelewa au kupata umaanisho wa tasfida hizi. Kwa mfano katika Ekegusii; '*otimokire*' kwa maana amepumzika, humanisha kifo. '*Otimokire*' kimkutadha yaweza kuwa ni kifo, kulala au kupumzika baadha ya kufanya shughuli za kila siku.

#### **2.4.3 Tasfida ng'amuzi na tasfida ng'amuzibwete**

Tasfida zikiwa chanya au hasi zaweza kuanishwa kama tasfida ng'amuzi na ng'amuzibwete. Tasfida ng'amuzi ni zile zilizoundwa zamani sana kwa sababu wanajamii wachache ndio huweza kukumbuka asili yao. Mara nyingi watu huzitumia bila kuwa na uelewa wao au bila kujua kama ni tasfida. Rowson (1991) anasema kuwa watu hutumia tasfida hizi bila kujua kama kuna kitu wanachokikwepa. Mifano katika lugha ya Ekegusii, '*gochiarooche*' yenye maana kwenda mtoni na '*korora omotienyi*' yenye maana kuona mwezi, hutumika kama tasfida za hedhi. '*Gotwa amate*' yenye maana kutema mate ni tasfida inayomaanisha kuenda haja ndogo. Hizi ni tasfida zimetumika tangu zamani. Wanaozitumia huona kama zina uhusiano wa moja kwa moja kwa kile zinazorejelea. Katika Kiswahili maneno kujisaidia, kwenda msalani na kujifungua hutumika.

Tasfida ng'amuzibwete ni changamano kwa sababu katika mawasiliano, msemaji huwa ana ufahamu wa tasfida hizo. Kwa hivyo huzitumia kwa uangalifu na kumfanya msikilizaji kuelewa ujumbe uliokusudiwa. Kwa mfano katika Ekegusii, '*gotwa amate*'

kumaanisha kutema mate hutumika kama tasfida ya kuenda haja ndogo badala ya neno kukojoa.

#### **2.4.4 Tasfida za misimu na tasfida endelevi**

Gatambuki (2009) anadai kuwa tasfida zaweza kuanishwa kwa uwezo wazo wa kudumu au kutokuwa na uwezo wa kudumu. Tasfida msimu ni tasfida ambazo kwa kuwa katika hali halisi tasfida zenyewe hazidumu bali hufifia au hujifia namna misimu inavyobadilika kiwakati. Kihistoria matumizi ya tasfida hizi yalikuwa ni kuepuka au kuficha mambo yahasuyo miiko na mbeko ya masuala ya kijamii. Inaaminika kuwa ni kutokana na hali hii ndio tasfida hutumika zaidi katika masuala yasiyozungumzwa hadharani kama vile kifo, magonjwa, tohara, harusi na pia mapenzi. Aidha tasfida msimu hutumika kuficha maneno yasiyokuwa na adabu na heshima. Pia huficha lugha isiyokuwa na adabu wala mbeko kwa kusudi la kuendeleza upole na kuhifadhi uso katika jamii husika. Kwa mfano katika Ekegusii, tasfida '*embura*' yenye maana 'mvua' hutumika kama neno la upole kumaanisha hedhi ili kuinga uso. Neno mwezi hutumika katika Kiswahili.

Tasfida endelevi vile vile ni zile ambazo hujimudu katika matumizi yake kwa muda mrefu. Kwa mfano katika lugha ya Ekegusii, neno '*ekebago*' yenye maana 'mpini' hutumika kama tasfida ya kurejelea sehemu nyeti ya mwanaume na neno '*omogondo*' hutumika kurejelea sehemu nyeti ya mwanamke. Tasfida hizi zimedumu kwa muda mrefu kiasi kwamba hutumika kama mazoea.

#### **2.4.5 Tasfida za kitaaluma**

Katika nchi nyingi ulimwenguni kazi za kiakili hushimiwa kuliko kazi za mikono. Hii ni kwa sababu kazi za mikono huonekana kuwa ni duni na hufanywa na watu wa tabaka la chini. Kazi za kiakili pia huvutia kwa kuwa wanaozifanya hulipwa mishahara minono. Tofauti hizi hutokana na kiwango cha mishahara. Hii huzua matumizi ya tasfida ili kutopujua uso kwa wale wanaofanya kazi duni. Kwa mfano katika Ekegusii, tasfida '*omoiseke*' yenye maana msichana hutumiwa badala ya neno '*omoreri*' lenye maana

yaya, kama njia ya kuonyesha upole kutokana na ile kazi yaya hufanya nyumbani hasa ya kushughulikia watoto.

#### **2.4.6 Tasfida za anatomia**

Kulingana na tasfida hizi, sio kila sehemu ya mwili wa binadamu huwa ni mwiko. Lugha inayohusishwa na viungo vya mwili ambavyo huhusika na ngono huweza kuangaliwa kwa aibu. Kwa hivyo huibua tasfida za viungo hivyo. Kwa mfano katika Ekegusii maneno haya hutumika '*enyimbo*' yenye maana fimbo kuashiria uume, '*gatigati*' yenye maana katikati kuashiria uke. Katika Kiswahili maneno kama vile *mkuki*, *kalamu na musumeno* hutumika kurejelea siri ya mume na *kitu* kurejelea siri ya mke. Tasfida zingine zaweza kuhusishwa na ulemavu, siasa, na kazi. Kutokana na hayo, ni kwamba kuna hali mbalimbali zinazozua matumizi ya tasfida. Baada ya kufafanua baadhi ya tasfida hizi, tunajadili hali mbalimbali zinazozua matumizi ya tasfida. Hali hizo ni pamoja na; mahusiano, dini, siasa magonjwa, kifo, sehemu za mwili na kujamiiana miongoni mwa hali zingine kama tutakavyofafanua ifuatavyo kwa kuzingatia upole kwa mujibu wa nadharia ya upole.

#### **2.5 Mahusiano miongoni mwa wanajamii**

Mahusiano ya kijamii huathiri jinsi watu wanavyotumia lugha. Hivyo basi watu hutumia maneno ya adabu na heshima kutegemea uhusiano uliopo kati ya msemaji na msikilizaji. Uhusiano huu pia huongozwa na misingi ya kitamaduni. Kwa hivyo mahusiano yaliyopo baina ya watu wanaotumia lugha ni muhimu katika uchambuzi na utambuzi wa masuala yanayozua matumizi ya tasfida. Mahusiano haya ni kama vile, mume na mke, mzazi na mwanawe, mtoto na mtoto mwingine, mheshimiwa na heshimiwa mwenzake au raia, mwanafunzi na mwalimu, kati ya wapenzi wawili na afisa mhalifu miongoni mwa mahusiano mengine. Kwa mfano, lugha inayotumika baina ya mzazi na mtoto huwa miiko ambayo huwaruhusu kuwasiliana kwa njia ya heshima. Leech (1983) anasema kuwa upole ni mkakati wa mawasiliano ambao watu hutumia kuanzisha na kuhifadhi mahusiano katika jamii. Aidha upole hudumisha mahusiano kupitia matumizi ya tasfida. Kila tasfida yaweza kutumika katika hali maalum mbali na kaida zingine za lugha.

Trudgil (2002:52) anasema kuwa mazungumzo ya jinsia tofauti, umri, na vyeo hutofautiana sio tu kwa hayo bali pia hutofautiana kulingana na muktadha wa jamii ambapo mzungumzaji hujipata. Katika hali hizi viwango vya umri, jinsia, hadhi vitahusika kama tutakavyofafanua.

### **2.5.1 Tofauti za kijinsia baina ya wanajamii**

Jinsia ni kiwango mojawapo cha mahusiano. Ni kigezo cha maumbile kinachodhihirisha kama mtu anayezungumziwa alizaliwa mume au mke. Dhana hii inahusiana na lugha kwa misingi ya matumizi ya tasfida. Marimadou (2000), Harry (1954), Hymes (2000) wanaonyesha kuwa tasfida huumbwa na na utamaduni wa jamii husika na hutegemea jinsi utamaduni ulivyomuumba binadamu wa kike na wa kiume. Lugha hugawika kutokana na masuala ya kijamii. Wanawake wanaaminika kutumia lugha ya adabu kwa kiwango kikubwa kuliko wanaume. Wanapotumia lugha ya adabu, wanachangia kuendeleza tasfida ambazo hudumisha upole katika mawasiliano na kuhifadhi nyuso. Uchunguzi wetu unalenga kutathmini jinsi tasfida hujishugulisha na masuala ya upole katika jamii.

### **2.5.2 Tofauti za umri baina ya msemaji na msikilizaji**

Katika mahusiano, watu walikomaa kiumri ndio wanaonekana kutumia tasfida kwa ufasaha kuliko watoto. Mawazo haya yanasawiana na Nguti (2012) ambaye anadai kuwa watu wazima ndio hutumia tasfida kwa kiwango kikubwa kuliko watu wa umri mdogo. Mbali na ukweli huu ni muhimu kufahamu kwamba watu wa umri sawa na jinsia moja wakati mwingi hawatumii tasfida lakini hii haimaanishi kuwa wanazua uchukivu mingoni mwao. Watu wa umri mmoja pia hutumia lugha inayofanana. Kwa mfano wazee hutumia mafumbo, taswira na methali ilhali vijana hutumia lugha nyepesi na inayoeleweka kwa urahisi. Njogu, Buliba na Mwiwaki (2006:61) wanasema kuwa katika mawasiliano baina ya wazee na vijana, vijana hutumia lugha ya adabu na heshima. Maneno kama vile ahsante, tafadhali, pole na kadhalika hutumika. Aidha vijana hupendelea lugha ya misimu kwa hivyo hutumia tasfida za misimu. Kwa mfano, vijana wanavyotumia neno '*kukatia*' kumaanisha kutongoza huwa wanahifadhi uso. Mathooko (2007:9) anadai kuwa mtoto hutumia lugha isiyokuwa ya tasfida. Kwa mfano mtoto

atasema “naenda kukojoa” ilihali mtu mzima atasema “naenda msalani au haja ndogo”. Hali hii huonyesha kwamba mtu hutumia lugha kulingana na umri wake.

### **2.5.3 Hadhi ya msemaji na msikilizaji**

Hadhi ni cheo alichopo mtu katika kazi anayoifanya. Hadhi vile vile huathiri matumizi ya tasfida. Watu wasio wa daraja moja hawana uhuru katika mazungumzo yao. Mazungumzo yao yana urasmi mwingi. Watu walio katika daraja moja wana uhuru mwingi hivyo wana heshima ya kiwango cha chini. Hii ni kwa sababu hawa ni watu wa daraja moja. Brown na Levinson (1987) wanasema kwamba kuna vipengele vitatu vya kisosholojia ambavyo huwafanya watu kuteua kiwango cha upole na kukadiria athari ya vitisho kwa uso katika mawasiliano. Vipengele hivyo ni pamoja na mamlaka, na mahusiano ya kijamii. Katika mazungumzo ya watu wasio wa daraja moja, kuna hali ya mhusika wa daraja la juu kuwa na satua na uwezo juu ya mwenzake wa daraja la chini. Kutokana na tofauti hizi, matumizi ya tafida huathirika kwa kiwango kikubwa hasa pale yule mwenye hadhi anapoamua ana mamlaka ya kusema mambo waziwazi na kwa hivyo si lazima kuwaheshimu wadogo wake.

Nguti (2012) anasema kuwa walio chini hutumia tasfida kwa sababu uongozi unafaa kuheshimiwa. Mawazo haya yanasawiana na yetu kwamba wanajamii huamini kuwa uongozi wowote ni lazima uheshimiwe, hali ambayo huwafanya walio chini ya uongozi kutumia lugha ya upole ili kuinga nyuso za wakubwa wao. Kutokana na hali hii ni kwamba uhusiano sawa huwapa msemaji na msikilizaji lugha maalum na uhusiano usio sawa huwapa msemaji na msikilizaji lugha maalum. Wanajamii hubuni maneno ya tasfida kuhusu watu walio nacheo aghalabu kuwaonyesha heshima. Kwa mfano katika Ekegusii maneno ‘*omogambi*’ lenye maana kiongozi ‘*omoruoti*’ yenye maana mfalme, ‘*omonene*’ yenye maana mkubwa hutumika. Katika Kiswahili maneno mkubwa, mheshimiwa, rais, mwinyi na mteule hutumika miongoni mwa majina mengine.

### **2.6 Tofauti ya kazi**

Watu wa jinsia tofauti hufanya kazi wakiwa pamoja. Katika hali hii huwa na mahusiano ya karibu. Mahusiano ni muhimu baina ya msemaji na msikilizaji. Msemaji



anapowasiliana na msikilizaji wake, uteuzi wake wa maneno utaelekezwa na uhusiano ulioko baina yao. Hivyo basi kuna vigezo vinavyomwongoza msemaji anapowasiliana. Vigezo hivyo ni kama vile, lugha anayoitumia, na mahali pake pa kazi. Mukaria (2011) anasema kwamba kazi afanyazo mtu huzua matumizi ya tasfida. Kwa mfano, wakili akiwa kortini atatumia lugha tofauti na ile anayotumia nyumbani. Lugha ya mtu kazini hutegemea na ile kazi anayoifanya. Aidha mahali ambapo lugha inatumiwa husababisha aina fulani ya matumizi ya lugha. Mathlani ofisini watu hutumia lugha rasmi. Mitagusano ya wafanyakazi kila siku huwapa fursa ya kuzoeana licha ya kuwa ni wa jinsia tofauti. Katika hali hii kiwango chao cha heshima hupungua. Hali hii huwafanya kutotumia lugha ya heshima bila kuvunjia wengine heshima yao. Lakini wakati ambapo uhusiano si wa karibu, inabidi lugha ya adabu na heshima kutumika. Matumizi ya tasfida huathirika pale ambapo watu wanaofanya kazi za kitaaluma hutaja maneno vile yanavyotumika. Hata hivyo hayatumiki kwa uchukivu wowote wala kukukwamiza mawasiliano au kupujua uso. Kutokana na hali, kuna uwezekano kuwa watu kazini wanaweza kutumia tasfida au wasituime lakini haimaanishi kwamba hawadumishi upole. Hivyo tasfida hutumika kulingana na kazi wazifanyazo watu.

## **2.7 Tofauti za kidini**

Illman (2005) anasema kwamba kila utamaduni una mambo ambayo hayazungumzwi wazi ambayo huitwa miiko. Mambo hayo hukatazwa kwa sababu za kidini au kitamaduni. Dini huathiri mielekeo ya lugha kwa kiasi fulani. Aghalabu kila dini huwa na lugha yao rasmi ambayo inatumiwa kuendesha shughuli zake. Katika dini ya ukristo watu hutumia maneno yanayohusiana na Mungu kwa njia ya heshima. Kwa mfano katika Kiswahili maneno '*baba, muumba, mtakatifu, na mwenyesi mungu*' hutumika kuonyesha heshima kwa Mungu ili kudumisha upole. Ekegusii pia maneno kama vile '*omonguru, omonda, omotongi*' ni bayana. Maneno hayo ni ya heshima anayopewa Mungu kuonyesha upole.

## **2.8 Hali za magonjwa miongoni mwa wanajamii**

Magonjwa huzua wasiwasi miongoni mwa wanajamii. Hii ni kwa sababu magonjwa ni ishara ya kifo. Kutokana na hali hii watu hutumia tasfida kuashiria magonjwa kusudi

kukinga uso wa waathiriwa. Kwa mfano katika Ekegusii maneno '*endwari*' yenye maana inayoleta madhara, '*enyamoreo*' yenye maana kukonda, na '*eng'iti enene*' yenye maana mnyama mkubwa hutumika kurejelea ukimwi. Katika Kiswahili maneno kama vile *nduli*, na '*mdudu*' hutumika kurejelea ukimwi. Kutokana na hali hii magonjwa pia huzua matumizi ya tasfida. Hata hivyo Njeri (2007) anadai kwamba si tasfida zote za magonjwa zinazoendeleza upole na kwa hivyo hukwamiza mawasiliano hasa pale ambapo msemaji na mpokeaji ujumbe wanatofautiana kiumri, uana na kazi wanazofanya.

## 2.9 Hali ya kifo

Kama tamaduni zingine ulimwenguni kwa wazungumzaji wa Kiswahili na Ekegusii, kifo kimepewa maana hasi kwa sababu kinahusishwa na shetani, tishio au bahati mbaya. Aidha watu wengi hufikiria kwamba wakitaja neno kifo moja kwa moja katika mawasiliano, maisha yao yamo hatarini au wanaweza kufa. Kwa hivyo wanajaribu wawezavyo kuepuka kutaja kifo moja kwa moja katika mawasiliano kwa kutumia tasfida. Hii ni kwa sababu tasfida hutumika kupunguza uchungu, huzuni na kuonyesha upole kwa waliofiwa. Kutokana na hali hii wameaunda maneno mengi ya upole yanayozungumzia kuhusu kifo. Hali hii pia hudhihirika katika Kiswahili na maneno kama kulala, kupumzika, kuenda hutumika kuashiria kifo. Katika Ekegusii maneno kama: '*korara*' - *kulala*, '*ochire*' - *ameenda*, '*orangeriwe*' - *ameitwa*, '*otimokire*' - *amepumzika*, '*otonyorire*' - *ametushinda*, '*otang'anire*' - *ametangulia* hutumika kuashiria kifo miongoni mwa tasfida nyingi ili kudumisha upole. Kutokana na hali hii ni bayana kwamba kifo kimepewa tasfida katika lugha hizi mbili.

## 2.10 Vitendo vya kujamiiana

Kujamiana ni suala la mwiko na kwa hivyo halisemwi hadharani kama suala la mjadala. Kutokana na hali hii tasfida nyingi zimebuniwa kuhusu kujamiana. Mukaria (2011) anasema kwamba suala la kujamiiana ni neno la aibu hasa mbele ya watu kwa hivyo huibua matumizi mengi ya sitiari. Mukaria akimnukuu Gatambuki (2009) anaelezea kwamba, tamaduni nyingi zina miiko kali inayotumika dhidi ya ngono nje ya ndoa. Allan na Burrige (1991) wanaeleza kwamba hii ni njia moja ya kuonya watu dhidi ya

uzinifu hasa wanawake. Ekegusii pia kama lugha zingine kina tasfida ambazo zimebuniwa na wanajamii kuhusu kujamiiana. Maneno kama vile *'obonyaka'* na *'obotomani'* ni tasfida zinazorejelea tendo la uzinifu. Pia maneno kama vile *'kororana'* yenye maana kuonana na *'koumerana'* yenye maana kukutana, ni tasfida zianazorejelea ngono. Katika Kiswahili maneno, *kujuana, kuonana na kukutana* hutumika kurejelea ngono kwa sababu yanakinga nyuso wa wahusika.

### **2.11 Taka ambazo hutoka mwili wa binadamu**

Hizi ni taka ambazo kwa kawaida binadamu hutoa kwa mwili na huwa zinaleta mkuruhu kwa watu. Kwa sababu takamwili hizi ni chanzo cha aibu, watu huepuka kuisema hadharani. Katika hali hii wanajamii hubuni maneno ya kufunika aibu hiyo kwa msemaji na msikilizaji. Allan na Burridge wanasema kwamba takamwili kama vile *kinyesi, hedhi na mkojo* huibua tasfida nyingi. Kwa mfano katika Ekegusii maneno kama *'kogenda eacha enke'* yenye maana kwenda haja ndogo, au *'gotwa amate'* yenye maana kutema mate ni tasfida zitumiwazo kurejelea haja ndogo. Pia *'gwekonya'* yenye maana kujisaidia hutumiwa kurejelea haja kubwa *'eubi'* yenye maana taka hutumika kurejelea kinyesi, *'embura'* yenye maana mvua hutumika kuashiria hedhi. Katika Kiswahili maneno kama kujisaidia, kwenda msalani, na kutema mate pia hutumika. Kutokana na mifano hii ni dhahiri kwamba takamwili huzua matumizi ya tasfida ili kukinga uso na kudhihirisha upole miongoni mwa wanajamii.

### **2.12 Sehemu za mwili**

Kimaumbile, mwanadamu ana sehemu za mwili ambazo hutekeleza majukumu tofauti tofauti. Hii ni kwa sababu kuna baadhi za sehemu za mwili ambazo hazisemwi hadharani kwa sababu zinaleta aibu. Hata hivyo sio sehemu zote za mwili hazisemwi hadharani. Mawazo haya yanasawiana na Mukaria (2011) anayesema kwamba sio sehemu zote za mwili ambazo ni mwiko. Anaongezea kwamba viungo vya mwili ambavyo huhusika katika ngono huweza kuangaliwakwa maudhiko na kwa hivyo huibua tasfida za viungo hivyo. Kwa mfano, *'ritimo'* yenye maana mkuki, *'omoswago'* yenye maana mchi, na *'ekebago'* yenye maana mpini ni tasfida zinazorejelea siri ya mume. *'Ekonu'* yenye maana kinu, *'omogondo'* yenye maana shamba na *'endagera'*

yenye maana chakula ni tasfida zinazorejelea siri ya mke. Hata hivyo katika Ekegusii sehemu kama vile makalio, na matiti hatajwa hadharani bila uchukivu wowote na hivyo hudumisha upole na kuendeleza mawasiliano. Ilihali maneno kama haya katika Kiswahili hayawezi kusemwa hadharani kwa kuwa yanaonekana kuwa ya aibu. Kwahivyo wazungumzaji hulazimika kuyatafutia tasfida kama vile 'maziwa' 'kibuyu cha mtoto' 'nyonyo' badala ya 'matiti' ili kuhifadhi uso wa mama mtoto.

### **2.13 Sherehe mbalimbali**

Sherehe mbalimbali kama vile harusi, tohara na mazishi miongoni mwa sherehe zingine ni mambo yanayohusiana na utamaduni. Kwa hivyo hayawezi kutenganishwa na jamii kwa kuwa jamii hutambuliwa kutokana na kaida, mila na desturi yao. Hymes (2000) anasema kuwa lugha ni jumla ya mitazamo, kaida, malengo na maadili yanayotambulisha asasi, shirika au kundi la watu. Katika hali hii, sherehe hizi ni kitambulisho cha jamii moja na nyingine. Ili kukwepa mambo yanayohusu miiko katika sherehe hizi, jamii ilibuni maneno ya heshima na adabu ili kudumisha upole. Ikumbukwe kwamba kila jamii ina mtazamo wake kuhusu sherehe hizi kwani sherehe hujukua nafasi kubwa na huthaminiwa miongoni mwa jamii mbalimbali. Jamii nyingi huwa zinatumia nyimbo ili kuakishi upole huu katika sherehe.

Hali halisi ni kwamba panapokuwa na mazungumzo katika lugha hizi mbili, hapakosekani tasfida kwa kuwa zinatumika kukinga uso wa mzungumzaji na msikilizaji. Ni kwa misingi hii ambapo tunaweza kusema kuwa kuna hali mbalimbali zinazozua matumizi ya tasfida katika lugha ya Kiswahili na Ekegusii. Aidha hali hizi hudhihirika katika lugha zote mbili licha ya kutofautiana kwa kiwango fulani. Ikumbukwe kwamba pia hali hizi huathiri matumizi ya lugha kwa ujumla.

### **2.14 Hitimisho**

Katika sura hii tumeshugulikia hali zinazozua matumizi ya tasfida katika Kiswahili na Ekegusii ili kuelezea upole katika mahusiano ya kijamii. Nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1978, 1987) ni namna ya kuelezea hali zinazozua matumizi ya tasfida katika mawasiliano ya kila siku ili kudumisha upole. Kwa kukabiliana na vitendo vinavyotishia nyuso za wahusika, tasfida hutumika katika hali mbalimbali. Hali hizi ni kama vile

mahusiano, magonjwa, dini, kifo, sehemu za mwili, kujamiiiana na takamwili. Tumetambua kwamba masuala yanayohusu uso na upole ni tofauti katika hali mbalimbali japo dhana ya hizi zinapatikana katika tamaduni zote ulimwenguni. Pamoja na ukweli huu tumeona kuwa tasfida zipo katika lugha zote mbili licha ya kuwepo tofauti fulani katika baadhi ya tasfida kimatumizi. Aidha tumeangazia dhana ya tasfida, historia na maendeleo yake. Pia tumebainisha tasfida mbalimbali za lugha hizi mbili. Kazi hii itakuwa mwongozo wa sura zitakazofuata.

## SURA YA TATU

### MCHANGO WATASFIDA KATIKA KUENDELEZA UPOLE

#### 3.0 Utangulizi

Baada ya kubainisha hali zinazozua matumizi ya tasfida, tutajadili jinsi tasfida zinavyochangia upole katika jamii. Tasfida ni kipengele cha lugha ambacho hutumika kufanikisha mawasiliano. Utovu wa upole ni mwiko miongoni mwa wanajamii. Tasfida hutumika kamachombo muhimu ambacho hukabiliana na mada ambazo hazizungumzwi hadharani. Pia hutumika na wanajamii katika kukabiliana na vitendo vinavyotishia nyuso za watu wengine. Hazitumiki tu kupunguza dhana ambazo hazitajwi hadharani katika jamii, bali pia hutumika kama chombo muhimu cha kuongeza upole na kuhifadhi nyuso za msemaji na msikilizaji ili kurahisisha mahusiano. Fraser (1990), Held (1992) na Watts (1992) wanasema kuwa upole huhusishwa na tabia na kaida za kijamii. Wanasema kuwa kuna uhusiano baina ya upole na vipengele vingine vya lugha katika mawasiliano ambapo tasfida ni mojawapo. Tasfida huhusishwa na upole kwa sababu lengo lake kuu ni kufanikisha mahusiano katika mawasiliano.

Lakoff (1991) na Brown na Levinson (1978, 1987) wanasema kwamba kutosema maneno moja kwa moja ni tabia njema ya kupunguza hali ya uchukivu na kukinga uso wa msemji na msikilizaji. Kutokana na hali hii, tasfida huhusishwa na uso kama alivyopendekeza Goffman (1967). Maneno ya upole huchangia kupunguza migongano na uchukivu katika mahusiano na mitagusano ya kila siku. Aidha maneno hayo yana uwezo wa kukinga uso kutokana na vitendo vinavyotishia uso. Tasfida, upole na uso ni mambo ambayo hayawezi kutenganishwa kwa kuwa lengo lao ni moja tu ambalo ni kudumisha mahusiano ya kijamii katika mawasiliano.

#### 3.1 Upole

Dhana ya upole imefanyiwa uchunguzi na wataalum wengi na kutolewa maelezo mbalimbali. Kila nadharia inayohusiana na dhana hii inatoa namna mbalimbali ya kutathimini upole katika mahusiano ya kila siku. Upole ni mkakati ambao watu hutumia kuanzisha na kuhifadhi mahusiano ya kijamii kama tulivyoeleza hapo mbeleni. Upole hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine kama zilivyo tamaduni. Mbinu mbalimbali

za upole hutumiwa ili kuokoa uso wamsikilizaji na msemaji tasfida zikiwemo. Kutumia upole ni njia moja ya kuboresha mahusiano baina ya watu na kuhakikisha kuwa mawasiliano yanaendelea bila kuvunjika.

### **3.2 Uhusiano baina ya tasfida na upole**

Tasfida kama mkakati wa upole, huhusishwa na usemi au maneno ya upole. Aidha ni mkakati wa upole unaopunguza vitendo vinavyotishia uso. Kwa sababu usemi huo hutokea katika diskosi ya kijamii, wanajamii huweka mbinu mwafaka ya kuhifadhi nyuso. Mahusiano katika jamii ni suala muhimu. Aidha kinachotambulikana kuwa ni tasfida katika lugha fulani, huenda ikawa si tasfida katika lugha nyingine. Katika utafiti wetu, tunachunguza mchango wa tasfida katika kuendeleza upole huu miongoni mwa wanajamii. Fraser (1990) ameeleza mitazamo minne kuhusu upole ambayo ni: mtazamo wa kaida za kijamii, mtazamo wa mazungumzo, mtazamo wa mkataba wa mazungumzo na mtazamo wa kuokoa uso. Tutaelezea mitazamo yote minne, japo katika uchunguzi wetu mtazamo wa kuokoa uso na mtazamo wa upole kama kaida ya kijamii ndio imejadiliwa kwa sababu mitazamo hii ndio hutumiwa kufafanulia mikakati ya upole katika mawasiliano katika tasfida za Kiswahili na Ekegusii.

### **3.3 Mtazamo wa upole kama kaida ya kijamii**

Kwa mujibu wa Fraser (1990), mtazamo huu wa kaida za kijamii huashiria uelewa wa kihistoria wa upole ambao umeshikiliwa na jamii mbalimbali. Mtazamo huu huchukulia kwamba kila utamaduni huwa na kaida za kijamii ambazo husheheni kanuni zinazoelekeza tabia fulani na hali ya mambo katika muktadha mahususi. Upole hutokea wakati ambapo kitendo fulani kinalingana na kaida za kijamii na utovu wa upole hubainika wakati kitendo hutendeka kinyume na kaida hizo. Kwa mfano katika jamii nyingi za Kiafrika ni mwiko mwanamke kutaja jina la baba mkwe au kupiga mluzi. Watoto pia hawataji majina halisi ya watu wazima hasa wazazi wao moja kwa moja. Pia ni kinyume cha kaida ya kijamii katika jamii nyingi za Kiafrika kurejelea sehemu za siri hadharani. Hali hizi hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Kutokana na mawazo hayo ni kwamba wazungumzaji wa Kiswahili na Ekegusii pia wana kaida mbalimbali ambazo huowaongoza na kaida hizi haziwezi kufanana moja kwa moja kwa kila hali.

Mtazamo huu wa upole kama jumla ya tabia nzuri na mbaya, ni dhahiri katika mawasiliano ya jamii japo kila jamii hutofautiana na nyingine katika kaida zake. Aidha mtazamo huu wa upole huonyesha upole kama dhana inayohusiana na namna ya kuzungumza ambapo kiwango kikubwa cha urasmi huashiria kiwango kikubwa cha upole baina watu katika mawasiliano. Huu mtazamo unahusiana na tasfida kwa kuwa tasfida hutumika kukuza heshima maadili na kuendeleza upole miongoni mwa wanajamii katika mawasiliano. Vile vile tasfida huhusishwa na kaida ya kijamii kwa kuwa kila jamii ina njia zake za kuhifadhi mahusiano yao kwa namna ya kutoathiri hisia chanya za watu. Hivyo huwafanya kuteua maneno yanayodumisha heshima katika mahusiano baina yao.

### **3.3.1 Upole kama mkakati wa mazungumzo**

Mtazamo huu huegemea kanuni za Grice (1975) aliyefafanua kuwa wasemaji humaanisha zaidi yawanayosema. Anadai kuwa haja ya wazungumzaji ni kupitisha ujumbe. Ili kuafikia lengo hili, alipendekeza kanuni ya jumla ya ushirikiano kama tulivyofafanua hapo awali.

Bila ushirikiano, itakuwa ni vigumu kwa watu kutagusano. Kwa hivyo kanuni za ushirikiano za Grice hutumika katika mitagusano ya mazungumzo kwa jumla. Wakati mwingine msemaji na msikilizaji huvunja kanuni hizi ili kukinga uso. Kanuni ya idadi inapovunjwa na kuhepa kauli za moja kwa moja husaidia kuhifadhi uso na kwa hivyo kuendeleza upole katika mawasiliano. Tasfida pia hutumiwa kama mbinu ya kupitisha ujumbe kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa lengo la kukinga uso.

Lakoff (1973) alitumia kanuni ya ushirikiano ya Grice katika kueleza dhana ya upole. Anadai kwamba matumizi ya lugha huongozwa na uwazi na upole. Anasema kwamba upole ni muhimu katika mawasiliano kwa lengo la kuepuka kumdhuru msikilizaji. Alieleza upole kama mbinu ya kuepuka migongano katika mahusiano. Kwa sababu hii alipendekeza kanuni ya uwazi na kanuni ya upole. Kanuni yake ya upole inasisitiza mahusiano ambayo hupunguza migongano katika mawasiliano baina ya wanajamii. Ili kupunguza migongano, aliigawa kanuni hii kwa vitengo vitatu kama ifuatavyo: kwanza, kutolazimisha ukweli, pili kutoa uhuru wa kuchagua na tatu kumfanya msikilizaji



kujihisi vizuri. Kanuni hizi huhusishwa na thamani na kaida za utamaduni. Mawazo haya pia yanawiana na (Maricic 2005). Mtazamo huu ni muhimu katika uchunguzi huu kwa sababu tasfida hutumika kupunguza migongano na mitafaruku baina ya wanajamii katika mawasiliano.

### **3.3.2 Kanuni ya mkataba wa mazungumzo**

Huu mkataba ulibuniwa na Fraser (1975) na Nolen (981). Upole unaangaliwa kama njia ya kutenda kazi kulingana na mahitaji ya mkataba wa mazungumzo. Fraser (1990:232) anasema kuwa wakati wazungumzaji wanapoanza mazungumzo yoyote, kila mshiriki huwa na uelewa wa utaratibu wa fulani wa haki na majukumu ambayo hubainiasha japo katika hatua za kimsingi, mambo ambayo wazungumzaji wanatarajia kutoka kwa kila mmoja. Anaongezea kuwa vigezo vya masharti mengine ya mkataba wa mazungumzo hulazimishwa na asasi za kijamii zinazohusishwa na mazungumzo husika.

Fraser anasema kuwa masharti mengine katika mtazamo huu yanabainika kupitia mitagusano ya awali ya msemaji na msikilizaji. Anasema kwamba kaida hizi hutofautiana katika kila mazungumzo na pia zinabadilika kulingana na utambuzi wa msemaji na msikilizaji katika mambo kama vile majukumu ya mzungumzaji, mamlaka na hadhi. Kwa mfano, kwa kawaida mtoto hana mamlaka juu ya mzazi wake. Kwa hivyo katika mtazamo huu upole unaangaliwa kama kushiriki katika mawasiliano kwa kuzingatia mkataba wa mazungumzo. Aidha ni mtazamo ambao hufanya mtu kujihisi vizuri kama anavyodai Leech na Lakoff. Ni mtazamo unaoendeleza mawasiliano. Mtazamo huu pia unahusishwa na tasfida ambazo hutumia lugha inayomfanya mtu kuhisi vizuri. Aidha ni mtazamo unaosaidia katika kuelewa jinsi tasfida hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Hii ni kwa sababu kila lugha ina kaida zake mbalimbali zinazowafanya wanajamii kutumia tasfida. Pia ni mtazamo unaotumika kuendeleza mawasiliano kama zilivyo tasfida. Kwa hivyo kwa kiwango fulani huhusishwa na tasfida.

### 3.3.3 Mtazamo wa kuokoa uso

Mtazamo huu wa kuokoa uso ndio umejadiliwa kwa kina katika kueleza dhana ya upole. Waasisi wa mtazamo huu ni Brown na Levinson (1978, 1978). Wanasema kuwa mikakati ya upole inayotumika katika mawasiliano inatofautina kutegemea ni nyuso gani za wahusika zinazohusika yaani nyuso chanya au nyuso hasi. Hii kauli inatiliwa mkazo na Fraser (1990:229) anaposema kwamba ni muhimu kwa msemaji kuhifadhi uso sio tu wake bali hata na nyuso za watu wengine. Uchunguzi wetu unaegemea mtazamo wa upole kama kaida ya kijamii na mtazamo wa kuokoa uso kama unavyoelezwa na Brown na Levinson (1978, 1987). Brown na Levinson walifafanua mikakati mbalimbali ya kuonyesha upole na kukinga uso. Mikakati hii husawiana na mikakati ya tasfida inayotumika kuendeleza upole na kukinga uso. Kwa hivyo tutajadili tasfida mbalimbali katika nyimbo za Kiswahili na Ekegusii. Tutatoa mifano mbalimbali ili kuonyesha jinsi tasfida hizo zinavyotumika katika mawasiliano kama mbinu ya kuokoa nyuso na kuendeleza upole miongoni mwa wanajamii.

### 3.4 Uchanganuzi wa data

Matumizi ya tasfida za Kiswahili na Ekegusii ni bayana na yamesawiriwa katika nyimbo za harusi za lugha hizi mbili. Tutajadili tasfida hizo kwa kuzitolea mifano kutoka kwa nyimbo zilizoteuliwa kuendeleza uchunguzi huu. Tutachanganua tasfida zilizo katika nyimbo za lugha hizi mbili na kuzilinganisha ili tuone jinsi zinavyokinga uso na kuendeleza upole katika jamii. Lugha inayotumika katika nyimbo husawiri matumizi ya tasfida ambazo hutumika kama mbinu mwafaka ya kuptisha ujumbe usiotajwa hadharani miongoni mwa wanajamii. Kwa hivyo tutajadili tasfida katika nyimbo zifuatazo:

#### Sherehe

*Wameringa kwa mahaba,*

*Wakiona la kushiba.*

*Kuolewa ni furaha*

*Sherehe hiyo ya harusi*

*Sherehe imeshatimia*

Katika wimbo 'sherehe' matumizi ya tasfida yanabainika katika ubeti wa tatu mshororo wa pili. Msemaji anasema, "wakiona la kushiba" Neno 'kuona' ni tasfida inayotumika kurejelea kujamiiana. Kujamiiana ni mwiko miongoni mwa wanajamii na huleta aibu. Kwa hivyo wanajamii hukwepa kukitaja hadharani na hivyo wanalazimika kutumia tasfida ili kuinga uso wa maharusi na watu wengine katika mawasiliano.

Katika wimbo huu neno 'kushiba' limetumika kufananisha mapenzi na njaa. Kama tulivyoeleza hapo mbeleni, sehemu ya siri ya mke hutasfidiwa kwa neno chakula. Kwa hivyo neno hili limetumika kuinga uso wa maharusi kutokana na aibu inayosababishwa na kitendo cha kujamiiana. Kauli hii haiathiri msikilizaji kwa sababu maneno kushiba na kuona ni ya kawaida katika mawasiliano ya kila siku. Msemaji anaposema kuolewa ni furaha ni njia moja ya kukwepa kutaja kitendo cha kujamiiana hadharani ili kuinga uso wa maharusi pamoja na hadhira. Aidha anapunguza uzito wa ukweli kuwa ndoa inawahusu mume na mke na wanafaa kushirikiana ili kuleta furaha katika ndoa. Kauli hii imetajwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa lengo la kuokoa uso na kuendeleza upole miongoni mwa wanajamii.

*Cheza cheza leo, umepata wako,*

*Bibi arusi cheza, leo umepata wako*

*Cheza leo umepata bwana, maneno hatuna,*

*Cheza hatuna maneno leo umepata bwana.*

Tasfida pia inadhihirika katika wimbo huu ubeti wa tano mshororo wa nne. Katika ubeti wa tano hapo juu msemaji anasema, "cheza hutuna maneno leo umepata bwana" Neno 'cheza' ambalo limetumika katika mshororo wa nne ni tasfida inayorejelea kitendo cha kujamiiana. Kwa kuwa kitendo cha kujamiiana ni mwiko, wanajamii hulazimika kutumia tasfida ili kupitisha ujumbe bila kuvunja au kukwamiza mawasiliano. Katika wimbo, huu neno hilo limetumiwa kuwashauri maharusi kufurahia mapenzi katika ndoa yao kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Katika hali ya kawaida wanajamii huchukulia kwamba kitendo cha kujamiiana ni mchezo unaotendeka baina ya mume na mke. Pia mume na mke ndio hushirikiana kuleta furaha katika ndoa. Neno cheza hutumika katika hali ya kawaida ya mawasiliano ya kila siku. Kwa hivyo linapotumika katika hali hii

huwa halisababishi uchukivu kwa msikilizaji au hadhira. Ni neno ambalo hutumika sio tu kukinga uso wa msikilizaji, bali pia nyuso za watu wengine katika mawasiliano.

Katika ubeti wa kwanza mshororo wa kwanza neno 'mahaba' ni tasfida inayotumika kurejelea mapenzi. Wanajamii katika mitagusano hukwepa kutaja mapenzi kwa njia ya moja kwa moja kwa kuwa huzua aibu mbele ya watu. Kutokana na hali hii, wanalazimika kutumia tasfida kama mbinu ya kuokoa uso.

### Pendo

Furaha yangu arusi imetimia

*Huyo ndiye wangu*

*Moyo ulomchagua'*

Picha, dhahabu pembeni kulia

*Sasa hauna la kulia*

Ni zawadi kwangu kutoka kwa mola

*Pendo limetimia*

*Mbele ya hadhira tumeshuhudiwa*

*Kwa mengi mola ametutendea*

*Leo hadharani twalitangaza pendo letu*

*Maana kwa imani tumetimiza pendo letu,*

*Mikono juu, vigelegele*

*Jamani si ni raha hiyo,*

*Bila huyu zitaweza,*

*Bila huyu siwezi,*

Wimbo 'pendo' pia umesawiri matumizi ya tasfida katika ubeti wa kwanza. Katika mshororo wa kwanza msemaji anasema, "picha, dhahabu pembeni kulia". Maneno 'picha na dhahabu' ni tasfida zinazotumika kumrejelea mwanamke. Aidha ni maneno ya heshima yanayotumiwa na mume kumtaja msichana katika siku ya harusi. Neno hili limetumika kukinga uso na pia kuonyesha heshima kwa bwana na bibi arusi.

Wimbo huu pia unadhihirisha matumizi ya tasfida katika ubeti wa pili mshororo wa kwanza. Msemaji anasema hivi, "Ni zawadi kwangu kutoka kwa mola". Neno 'zawadi' katika ubeti huo ni tasfida inayotumika kumtaja mke. Katika harusi, neno hili hutumiwa kumsifia bibi arusi. Msemaji ametumia neno hili ili kukinga uso wa bibi arusi. Aidha ni neno ambalo hutumika kuendeleza upole katika mawasiliano.

### Ndoa

*Kutizama hali ni jambo sawia,*

*Kwa walo tayari kuifunga ndoa,*

*Ukiwa tajiri usioweza tulia,*

*Waweza tulia ukishapata bibi bikira*

*Tamaa yako Ali ni yenye wasaa,*

*Ki pato halali unategemea,*

*Maradhi ya mwili yaweza tulia,*

*Ukipata mwenye utakayemuoa*

*Iwapo fakili mnapokutana,*

*Chakula halali huwezi kutoa*

*Kwako hukijali huwezi kumwambia,*

*Wewe si halali na mmefunga ndoa*

Katika wimbo 'Ndoa' ubeti wa pili mshororo wa tatu msemaji anasema, '*maradhi ya mwili yaweza tulia*'. Neno '*maradhi*' ni tasfida inayotumika kurejelea mapenzi. Hali ya mapenzi katika jamii huwa haitajwi moja kwa moja kwa kuwa ni mwiko. Ili kukwepa aibu inayosababishwa na kitendo cha mapenzi, wanajamii hulazimika kutumia tasfida kama mbinu mbadala ya kutaja kitendo hicho hadharani bila kuwavunjia watu heshima wala kuvunja mawasiliano. Kutumia neno hili pia ni njia ya kuwa mpole katika mahusiano. Katika wimbo huu neno hili limetumika kuinga uso wa bwana harusi. Aidha ni neno ambalo limetumika kumshauri bwana harusi kuhusu mapenzi kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Mapenzi yanafananishwa na maradhi ya mwili ambayo huponywa na mke. Pia neno hilo limetumika kudumisha upole miongoni mwa wanajamii na kuendeleza mawasiliano.

Katika ubeti wa huo huo wa pili mshororo wa pili, msemaji anasema hivi: "*kipato halali unategemea*". Neno '*kipato*' ni tasfida inayotumika kumrejelea mke. Katika mawasiliano na mitagusano ya kila siku, neno hili hutumika kama neno la kawaida katika lugha. Kipato ni faida apatayo mtu kutokana na kazi fulani. Hivyo neno hilo linapotumika katika harusi, ni njia ya upole ya kumfahamisha mume kwamba amepata mke halali na mahitaji yake ya kimwili yatashugulikiwa. Kwa kuwa hawezi kuambiwa hadharani, neno hili kipato hutumika kuokoa uso. Aidha neno hili hutumika kupunguza aibu miongoni mwa watu. Ni neno limetumika kuendeleza upole unaohitajika miongoni mwa wanajamii katika mawasiliano.

Wimbo huo pia umedhirisha tasfida katika ubeti wa tatu mshororo wa pili ambapo msemaji anasema hivi "*chakula halali huwezi kutoa*". Neno '*chakula*' kama linavyotumika katika usemi huu ni tasfida inayorejelea sehemu ya siri ya mke. Ni neno ambalo hutumika kufunika aibu ya kutaja siri ya mke hadharani kwa njia ya moja kwa

moja. Wanajamii hutumia neno hili sio tu kukinga uso wa mke, bali pia kukinga nyuso za watu wengine. Pia hutumika kuendeleza upole na kufanikisha mawasiliano.

### Upendo

*Wakati wawili wanapooana,*

*Wao ni sawa na mito miwili inayokutana mahali pamoja,*

*Ili kutengeneza mto mmoja,*

*Maji hayo hayawezi kuwa matulivu wakati wa mwanzo mwanzo,*

*Lakini kadiri yanavyoendelea kutiririka,*

*Yatatulia kabisa ooh*

Katika wimbo ‘Upendo’ ubeti wa kwanza mshororo wa pili msemaji anasema, “*wao ni sawa kama mito miwili inayokutana mahali pamoja*”. Neno ‘mito’ ni tasfida inayorejelea wapenzi. Aidha ni tasfida inayorejelea kujamiiana. Msemaji ametumia neno mito kuwafananisha wapenzi wawili. Kwa kuwa kitendo cha mapenzi huleta aibu miongoni mwa wanajamii, neno ‘mito’ limetumika kukinga uso wa maharusi. Aidha ni neno ambalo limetumika kuendeleza upole katika mawasiliano baina ya watu.

*Furaha huwa nzuri katika ndoa,*

*Mfurahie mwenzi wako wakati wowote,*

*Mshirikiane na umwambie nakupenda,*

*Muone kama mmekutana mara ya kwanza,*

*Mwambie nakupenda*

Katika wimbo huu ubeti wa tatu mshoro wa tatu msemaji anasema hivi, “*mshirikiane na umwambie na kupenda*”. Neno ‘kushirikiana’ ambalo limetumika ni tasfida inayorejelea kujamiiana. Kwa kuwa kujamiiana ni mwiko miongoni mwa wanajamii, neno kushirikiana limetumika kukinga nyuso za maharusi na nyuso za hadharani za wanajamii.

Katika wimbo huu huu ubeti wa nne mshororo wa nne, msemaji anasema hivi, “*muone kama mmekutana mara ya kwanza*”. Neno ‘*kuona*’ katika usemi huu ni tasfida inayorejelea kitendo cha kujamiiana. Kitendo cha kujamiiana hakitajwi moja kwa moja katika mawasiliano kwa sababu huzua aibu mbele za watu. Ili kukwepa aibu, wanajamii hutumia neno ‘*kuona*’ kuinga nyuso sio tu za maarusi, bali pia nyuso za wanajamii. Kwa kuwa ni neno ‘*kuona*’ ni la kawaida katika lugha, haliwezi kuzua aibu baina ya watu katika mawasiliano. Kauli hii pia imetumika kama njia ya kuendeleza upole na kuhifadhi heshima inayohitajika baina wanajamii. Katika hali hii msemaji anajaribu kuinga nyuso za wahusika na kuongeza upole katika mawasiliano.

Katika ubeti huo neno ‘*kukutana*’ katika mshororo huo huo limetumika katika usemi huu kama tasfida ya kurejelea kitendo cha kujamiiana. Kwa hivyo maneno *kuona* na *kukutana* yametumika kuinga nyuso za maarusi na vile vile kuendeleza upole katika mawasiliano.

### Harusi

*Kama mungu alivyoipenda kanisa,*

*Ndivyo mume umpende mke wako,*

*Mke hapiwi kama gumbigumbi,*

*Anatulizwa na maneno matamu*

Wimbo harusi pia umesawiri matumizi ya tasfida. Katika ubeti wa pili, mshororo wa tano na sita msemaji anasema hivi, “*kama kristo alivyoipenda kanisa, ndio mume umpendemke wako*”. Neno ‘*kanisa*’ ni tasfida inayotumika kumrejelea mke. Mwanamke hufananishwa na kanisa kwa kuwa ni mahali pa kumwabudu mungu. Huu usemi umetumika kuwashauri maharusi kudumisha upendo katika ndoa. Msemaji anakwepa kutaja kauli hii kwa lugha ambayo inaweza kusababisha athari hasi au uchukivu kwa msikilizaji. Aidha kanisa ni neno la heshima linalotumika kumtaja mke. Tasfida hii imetumika kudumisha upole katika mwasiliano na kuinga nyuso za wanajamii.

*Nawe mke mtii mume wako,*

*Mpe heshima na kila kitu.*



*Naye mume atafurahi,*

*Mshirikiane katika ndoa.*

*Naye mungu atawabariki awape amani,*

Katika ubeti wa tatu mshororo wa pili hapo juu, msemaji anaonyesha matumizi ya tasfida. Anasema, “*mpe heshima na kila kitu*”. Neno ‘*kitu*’ ni tasfida inayorejelea siri ya mke. Sehemu hii ni mwiko miongoni mwa wanajamii na kwa hivyo huwa haitajwi hadharani kwa kuwa inaweza kuzua aibu kwa msemaji na msikilizaji. Neno hili limetumika kumshauri bibi arusi kumheshimu na kumtimizia mume wake mahitaji yake ya kimwili ili kuleta furaha katika ndoa. Kutokana na aibu inayosababishwa na sehemu hii, msemaji hutumia tasfida hii kutaja sehemu hiyo hadharani pasipo kuvuruga mahusiano wala kuvunja mawasiliano. Tasfida hii imetumika kwa lengo la kukinga uso wa bibi arusi na kudumisha upole baina ya msemaji na msikilizaji.

Katika wimbo huu ubeti wa pili mshororo wa tatu mesemaji ametumia usemi huu, “*mshirikiane katika ndoa*”. Neno ‘*kushirikiana*’ ni tasfida inayotumkia kurejelea kujamiiana. Tasfida hii imetumika kuwashauri maharusi kutimiza mahitaji ya kimwili ili kudumisha ndoa. Tasfida hii imetumika kukinga nyuso za maharusi na pia kudumisha upole katika mawasiliano.

*Sirori*

*Sirori, sirori my dear,*

*Eng’ombe nyamagoro ane,*

*Nero yang’ura yuu,*

*Sirori my dear*

*Enyangi yomotangi.*

*Naki ndakore morore?*

*Omwanchi twanchaine.*

*Baka enkoro ime*

*Twabangire enyangi.*

*Enyangi yebitinge,*

*Asibwe nebitinge*

*Ekeru togoara,*

*Igo are maridadi*

*Amaiga akona kondia,*

*Naki ndakore morore?,*

*Rituko erio rienyangi,*

*Rituko nario rero*

*Kindoche omwanchi one,*

*Are nomogoko*

*Ee ninde nomogoko,*

*Rituko nario rero,*

*Kori kori x2 kori maguta kori,*

*Kori maguta kori,*

*Omosuko ntakorochi*

*Amariga akona goita*

*Narero iga oyeee x2*

*Omosuko ntakorochi*

*Amariga akona goika*

*Baba gachi mogondo x2*

*Gosimeka ching'ende,*

*Narero iga oyee*

*Omosuko ntakorochi*

*Amariga akona goika*

***Tafsiri ya Kiswahili***

*Sirori sirori my dear,*

*Ng'ombe yenye miguu minne,*

*Ndio imenipokonya mpenzi,  
Sirori sirori mpenzi*

*Arusi ya kifungua mimba,  
Nitafanyaje nimwone,  
Namuota kila siku,  
Mpenzi tunapendana,  
Mpaka ndani ya roho,*

*Tumepanga harusi,  
Harusi ya ebitinge,  
Afungwe ebitinge  
Wakati tunapotembea,  
Anaonekana mrembo kweli,  
Nataka kumsalimia,  
Nitafanyaje nimwone,*

*Siku hiyo ya harusi,  
Siku ndio leo,  
Nikimwona mpenzi wangu,  
Akiwa na furaha,  
Eee nina furaha,  
Siku ndio leo,*

*Kori x2 kori mafuta kori  
Kori mafuta kori  
Wakati sikuoni machozi yanidondoka*

*Mama enda shambani,  
ukapande maharagwe,  
Na leo hivi oyee,*

### *Wakati sikuoni oyee' machozi yanidondoka*

Katika wimbo 'sirori', msemaji ametumia tasfida. Ubeti wa pili mshororo wa kwanza msemaji anasema hivi, "enyangi yomotangi". Neno 'omotangi' (kifungua mimba) ni tasfida inayotumika kumrejelea mke. Aidha ni neno la heshima ambalo hutumiwa na mume kumtaja mke wake. Katika wimbo huu neno hili limetumiwa kumsifia bibi arusi. Katika mahusiano baina ya mume na mke, neno hili linatumika kuhifadhi uso wa bibi arusi. Pia wanajamii hutumia tasfida hii ili kukwepa kutaja neno mwanamke moja kwa moja kwa sababu neno halisi huonekana kuzua uchukivu. Aidha ni neno linadhihirisha ukosefu wa heshima kwa wanawake linapotajwa vile lilivyo. Ili kukwepa uchukivu huu, wanajamii hulazimika kutumia tasfida kwa lengo la kuinga nyuso za wanawake.

Katika wimbo huo huo ubeti wa pili mshororo wa nne msemaji anasema, "omwanchi twanchaine" (mpenzi tunapendana). Neno 'omwanchi' (anayependa) katika wimbo huo ni tasfida inayotumika kumrejelea mume au mke. Hasa neno hili hutumiwa na maharusi, wachumba au mtu na mkewe kama njia ya kuonyeshana heshima na upendo miongoni mwao. Neno hili huwa halitajwi na wanajamii mahali popote au wakati wowote kwa kuwa ni neno linalotumiwa baina ya mume na mke. Katika wimbo limetumiwa kuwahimiza bwana na bibi arusi kuheshimiana na kupendana katika ndoa.

Kwa upande mwingine neno hilo laweza kutumiwa kama tasfida ya kurejelea mapenzi kwa njia isiyo ya moja kwa moja baina ya mke na mume. Kwa hivyo limetumika kuinga nyuso za maharusi kwa kuwa wangeaibika iwapo wangeambiwa hadharani. Kwa hivyo limetumika ili kuepuka kupujua uso. Hata hivyo kuna baadhi ya maneno katika Kiswahili kama vile 'mpenzi' ambayo hutajwa vile yalivyo bila kutasfidiwa lakini bado yanadumisha upole baina ya msemaji na msikilizaji. Maneno hayo hayo hutafutiwa tasfida katika lugha ya Ekegusii. Kutosema kauli kuhusu mapenzi kwa njia ya moja kwa moja ni mbinu ya kuinga nyuso za maharusi na pia watu wengine.

Katika ubeti wa tano mshororo wa pili msemaji anasema hivi, "Kori maguta Kori". Neno 'maguta' (mafuta) ni tasfida inayomrejelea mke. Neno hili hutumika kumsifia bibi

arusi siku yake ya harusi. Bibi harusi hufananishwa na chombo laini na nyororo. Tasfida hii hutumika kuonyesha upole na kuhifadhi nyuso za hadharani.

Katika ubeti wa tatu mshororo wa kwanza msemaji anasema, “*twabangire enyangi*”. Neno ‘*Enyangi*’ ambalo limetumika katika usemi huo ni tasfida inayorejelea mapenzi. Neno hili limetumika ili kukinga nyuso za maharusi. Aidha limetumika kudumisha upole unaohitajika baina ya wanajamii katika mawasiliano.

Mfano mwingine wa tasfida unabainika katika ubeti wa pili mshororo wapili na ubeti wa nne mshororo wa pili msemaji anasema, “*Naki ndakore morore?* (Nitawezaje kumwona?). Swali hili halihitaji majibu kwa kuwa ni swali balagha. Neno ‘*komorora*’ (kumwona) ni tasfida inayorejelea kujamiiana. Kitendo cha kujamiiana ni mwiko kwa hivyo huwa hakitajwi hadharani kama tumeeleza hapo awali. Katika wimbo huu, neno hilo limetumika kuficha aibu inayosababishwa na kitendo cha kujamiiana. Aidha neno hilo limetumika sio tu kukinga nyuso za maharusi, bali pia nyuso za wanajamii. Limetumiwa ili kuhakikisha kwamba mawasiliano hayavunjiki baina ya watu. Aidha ni neno ambalo huendeleza upole unaohitajika katika mawasiliano.

Wimbo huu pia umesawiri matumizi ya tasfida katika ubeti wa tano mshororo wa pili na wa tatu. Msemaji anasema hivi, “*mama gachi mogondo, gosimeka chingende*”. Neno ‘*mogondo*’ (*shamba*) ni tasfida inayorejelea sehemu ya siri ya mke. Kulingana na jamii, sehemu ya siri ya mke haitajwi hadharani kwa sababu huzua aibu mbele ya watu. Ili kukwepa aibu ya sehemu hii, wanajamii hulazimika kutumia tasfida hii ili kukinga nyuso za wanawake na pia za watu wengine katika mawasiliano.

Aidha neno ‘*gosimeka*’ (kupanda) ni tasfida inayorejelea kuwa mjamzito. Katika wimbo huu tasfida hii imetumika kumfahamisha bibi arusi kwa njia ya upole kwamba baada ya harusi wanajamii wanamtarajia kupata watoto. Kwa hivyo ni tasfida inayotumika kukinga uso wa bibi arusi kutokana na aibukwamba mimba hutokana na kitendo cha ngono. Ili kukwepa aibu inayosababishwa na kitendo cha kujamiiana, wanajamii

hulazimika kutumia tasfida ili kuokoa uso na kuendeleza upole miongoni mwa wanajamii.

**Kwaeri**

*Kwaeri Nyandego,  
Bono nkogenda tore,  
Kwaeri nyandego,  
Ee bono nkogenda tore,*

*Nachigotiria etiriri,  
Nkanyora nabuire,  
Kwaeri omongwana,  
Bono nkogenda tore,*

*Nachi goteka ogoteka,  
Nkanyora yanyure,  
Kwaeri omongwana,  
Bono nkogenda tore,*

***Tafsiri ya Kiswahili***

*Kwaheri Nyandego,  
Sasa tunaenda,  
Kwaheri nyandego,  
Eee sasa tunaenda,*

*Nimerukaruka mchezo,  
Nimepata nimeshinda,  
Kwaheri muungwana,  
Sasa tunaenda,*

*Nimeteka kuteka,*

*Nikapata imeingia,  
Kwaheri mpenzi,  
Sasa tunaenda.*

Katika wimbo ‘*Kwaeri*’ ubeti wa kwanza mshororo wa pili msemaji anasema hivi, “*Bono nkogenda tore*” (sasa tunaenda) Neno ‘*okogenda*’ katika usemi huu ni tasfida inayoashiria kuolewa. Neno hili limetumika kama njia ya upole ya kumfahamisha msichana kuwa wakati wake wa kuolewa umefika. Pia limetumika kumpa msichana kwaheri kwa njia ya upole anapoenda ugenini kuungana na jamii nyingine asihisi upweke. Kitendo cha kuolewa hakitajwi moja kwa moja. Hii ni kwa sababu kuolewa kunahusishwa na huzuni kwa jamii ya msichana ambayo inamtoa binti wao kwa jamii ya nyingine ya mbali na furaha kwa jamii ya mvulana. Kutokana na hali hii wanajamii walibuni tasfida ili kukwepa hatari inayosababishwa na kitendo cha kuolewa. Pia ni njia kuinga uso na kudumisha baina ya watu.

Wimbo huu pi umedhihirisha matumizi ya tasfida katika ubeti wa tatu mshororo wa pili, msemaji anasema hivi “*nachi goteka ogoteka*”. Neno ‘*ogoteka*’ (kuteka) ni tasfida inayorejelea ngono. Tasfida hii hutumika kutajia kujamiiiana hadharani bila kuvuruga wala kukwamiza mawasiliano. Vile vile hutumika kuinga nyuso za maarusi. Hii ni kwa sababu watu huelewa kiini cha ndoa baada ya harusi. Pia ni tasfida inayotumika kuendeleza upole katika mawasiliano kwa kuwa kuteka ni neno la kawaida katika lugha linatumiwa katika michezo.

Katika wimbo huo huo ubeti wa nne pia matumizi ya tasfida yamebainika. Msemaji anasema hivi, “*nachi gotiria etiriri*”. Usemi ‘*gotiria etiriri*’ (kucheza mchezo) ni tasfida inayorejelea kujamiiiana. Tasfida hii hutumika kuinga nyuso za maarusi na pia kuendeleza upole unohitajika miongoni mwa wanajamii katika mwasiliano.

Katika wimbo huu ubeti wa nne mshororo wa tatu neno ‘*konywa*’ (kufungwa bao) ni tasfida kuwa mjamzito. Ni tasfida inayotumika kufahamisha bibi arusi kwamba baada ya arusi anahitajika kupata watoto. Neno hili hutumika kuinga uso wa bwana na bibi arusi na pia kudumisha mawasiliano.

Neno 'omongwana' (muungwana) katika ubeti wa nne mshororo wa tatu ni tasfida inayorejelea jina la kijamii. Hili ni neno la heshima linalotumiwa kumtaja mume katika siku yake ya harusi. Hivyo ni tasfida inayodumisha upole katika mawasiliano.

### **Ekeru okogenda**

*Osebe ekeru okogenda,*

*Ondangerie ngokobe*

*Osebe ekeru okogenda,*

*Ondangerie ngokobe*

*Switi switi banana*

*Egetenga kieritoke*

*Abagaka inchuo tomane chiombe,*

*Ee rituko nario eri x2*

*Switi switi banana*

*Egetenga kieritoke x2*

### **Tafsiri ya Kiswahili**

*Osebe utakapoenda,*

*Unite nikizindikishe,*

*Switi switi banana,*

*Mgomba wa ndizi,*

*Wazee njoo tuchukue mahari,*

*Siku ndio hii,*

*Switi switi banana,*

*Mgomba wa ndizi*

Ubeti wa pili mshororo wa kwanza unasawiri matumizi ya tasfida. Msemaji anasema hivi, "abagaka inchuo tomane chiombe". Neno 'abagaka' ni tasfida inarejelea wanaume wakubwa kwa umri. Hili ni neno la adabu linalotumika kuwarejelea waliokomaa umri



kuonyesha adabu na heshima. Katika muktadha huu neno hili limetumika kuendeleza upole na mahusiano mema miongoni mwa wanajamii.

Katika ubeti wa huo pili mshororo wa nne msemaji anasema, “*egetenga kiritoke*”. Neno ‘*egetenga*’ ni tasfida ya inayotumika kumtaja mwanamke. Aidha ni neno ambalo hutumika kuonyesha adabu na heshima kwa bibi arusi. Matarajio ya wanajamii ni kwamba msichana anapolewa atabarikiwa na watoto. Ili kumwambia apate watoto wengi kwa njia isiyo ya moja kwa moja, wanajamii hulazimika kutumia tasfida. Kutokana na hali hii wanajamii walitumia neno hilo kukinga uso wa bibi arusi wanapomshauri apate watoto wengi kuendeleza kizazi. Pia neno hili linapotumika, huonyesha upole katika mahusiano baina ya watu. Neno hili halitumiki tu kukinga uso wa maarusi, bali pia hutumika kukinga nyuso za wanajamii na kuendeleza upole katika mawasiliano.

Katika ubeti wa kwanza mshororo wa pili msemaji anasema, “*ekero okogenda*” neno ‘*okogenda*’ vile tumeeleza hapo mbeleni ni tasfida inayorejelea kuolewa. Tasfida hii imetumika kukinga uso wa bibi arusi na pia kudumisha upole katika mawasiliano.

### *Mbwangonde*

*M’boera ee ee, x2*

*M’boera m’bwangonde ng’ende,*

*Ng’a omogoye m’boere richambe.*

### ***Tafsiri ya Kiswahili***

*Nifungi eee ee,*

*Nifungie haraka niende,*

*Nipe kamba nifungie mkeka*

Katika wimbo huu ubeti wa kwanza mshororo wa pili msemaji anasema, “*mboera eee ee*” Neno ‘*mboera*’ (*nifungie*) ni tasfida inayorejelea kitendo cha kujamiiiana. Kwa kawaida baada ya harusi, wanajamii hutarajia mke na mume kujamiiiana. Kwa sababu kitendo cha kujamiiiana ni mwiko, wanajamii walikwepa kutaja kitendo hicho moja kwa

moja ili kukwepa aibu. Kutokana na hali hii walibuni tasfida 'mboera' (nifungie) ili kutaja kitendo cha kujamiiana hadharani bila kuvuruga au kuvunja mawasiliano. Neno hili hutumika kukinga uso wa bibi arusi na nyuso za hadharani za wanajamii.

Katika ubeti wa kwanza mshororo watatu usemi "*Nga'a omogoye mboere richambe*" (nipe kamba nifungie mkeka). Usemi huu umetumika kuwahimiza maharusi kwamba wanafaa kushirikiana katika kutimiza mahitaji ya kimwili. Neno 'omogoye' (kamba) ni tasfida inayorejelea siri ya mume. Kwa hivyo usemi huu umetumika kuokoa uso wa bwana arusi. Aidha neno hili limetumika ili kuhifadhi nyuso na mahusiano baina ya wanajamii. Katika jamii sehemu ya siri ya mume huwa haitajwi moja kwa moja kwa kuwa ni mwiko. Neno hili limetumika kupunguza uchukivu unaoletwa na neno la mwiko. Katika wimbo huu neno hili limetumika kudumisha heshima ya wanajamii katika mawasiliano.

### **Obwanchani**

*Bwabokire, bwabokire obwanchani,*

*Bwabokire, bwabokire obwanchani,*

*Bori bwa kare, bori bwakare obwanchani,*

*Ekeru narengi omwana,*

*Obe nkaniwa baba,*

*Obe nkaniwa eee,*

*Nkaniwa timbasa koria amara a baba,*

*Nkoria amara, obe ng'a nintamue*

*Ekeru nainyoiri tata agantebia,*

*Moisia gachi orisie,*

*Ndisia omobaso boira'*

*Ngacha gotiga ee*

### ***Tafsiri ya Kiswahili***

*Umeanza upendo, umeanza upendo,  
Umeanza upendo, umeanza upendo,  
Ule wa zamani, ule wa zamani,*

*Nilipokuwa mtoto obe, nilikatazwa na mama,  
Obe, nilikatazwa,  
Nizile change eee,  
Nikila nitakuwa mtoro,  
Obe, nitakuwa mtoro,*

Katika wimbo ‘*obwanchani*’ ubeti wa nne mshororo wa nne msemaji anasema, “*moisia gachi orisie*” Neno ‘*korisia*’ ni tasfida inayorejelea kuchumbia. Tasfida hii imetumiwa kumshauri mvulana kuwa amefika umri wa kumtafuta mchumba au kuoa. Kwa hivyo anajulishwa kuwa anastahili kuoa kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Neno hili hutumiwa kwa lengo la kukinga uso na kudumisha upole katika mawasiliano.

Wimbo huu pia umesawiri matumizi ya tasfida katika ubeti wa nne mshororo wa nne. Msemaji anasema hivi “*moisia gachi orisie*”. Neno ‘*miosia*’ limetumika kama tasfida ya mahusiano. Neno hili hutumiwa na wanaume waliokomaa kuwatajia vijana waliofika umri wa kuoa. Tasfida hutumika kukinga uso wa mvulana na pia kuendeleza upole anaposhauriwa kuwa amefika umri wa kuolewa bila kuvunja mawasiliano. Neno ‘*baba*’ katika ubeti wa pili mshororo wa nne na neno ‘*tata*’ katika ubeti wa tatu mshororo wa kwanza kama yanavyotumika ni tasfida zinazorejelea mahusiano miongoni mwa wanajamii.

Katika wimbo huu huu ubeti wa kwanza mshororo wa kwanza msemaji ametumia neno “*obwanchani*”. Neno hili ni tasfida inayorejelea kitendo cha kujamiiana. Kujamiiana ni mwiko miongoni mwa wanajamii. Ili kukwepa kutaja kitendo hiki moja kwa moja tasfida hii inatumika ili kuokoa nyuso za maharusi na pia nyuso za watu wengine. Aidha ni njia ya kuendeleza upole miongoni mwa wanajamii.

Kutokana na mifano ambayo tumetoa, ni dhahiri kwamba tasfida zipo katika lugha zote mbili. Ulinganifu umeonekana kwa kiasi katika tasfida za lugha hizi. Tumetambua kwamba tasfida nyingi ambazo zimejitokeza katika lugha za Ekegusii na Kiswahili zianakaribiana. Hii ni kwa sababu hakuna lugha mbili zinazoweza kufanana katika kila hali. Pia tumetambua kwamba baadhi ya maneno ambayo ni tasfida katika lugha ya Ekegusii si tasfida katika lugha ya Kiswahili.

Tofauti iliyoko baina ya tasfida za lugha hizi mbili ni kwamba baadhi ya maneno yanayohusu ndoa yanatajwa bila kutasfidiwa katika lugha ya Kiswahili lakini bado yanadumisha upole. Kwa upande mwingine maneno hayo hayo katika Ekegusii lazima yatafutiwe tasfida. Hii ni kwa sababu kila watumizi lugha wana njia tofauti za kuteua tasfida zao na tasfida hizo hutumiwa kwa njia ya kipekee. Kutokana na kauli hii ni kwamba sio maneno yote yanayotasfidiwa katika lugha ya Ekegusii yanaweza kutasfidiwa katika lugha ya Kiswahili. Aidha neno linaloonekana kuwa la upole katika lugha ya Ekegusii huenda ikawa si la upole katika lugha ya Kiswahili.

Pia tumetambua kwamba Ekegusii kimesawiri matumizi mengi ya tasfida katika nyimbo za harusi. Imebainika kwamba kuna baadhi ya maneno yanayotasfidiwa katika nyimbo za harusi za Ekegusii na maneno hayo hayo yanatajwa vile yalivyo katika nyimbo za harusi za Kiswahili. Hii inadhihirisha kwamba neno ambalo ni tasfida katika lugha moja huenda ni kinyume katika lugha nyingine. Aidha tumetambua kwamba licha ya kuwa baadhi ya tasfida katika nyimbo za lugha zote mbili zinatofautiana, bado zinatumiwa kuingia uso na kuendeleza upole miongoni mwa wanajamii. Kutokana na hayo ni kwamba tasfida ni kipengele muhimu cha lugha ambacho huchangia pakubwa katika kuongeza upole katika jamii. Isitoshe, upole hauwezi kuendelezwa pasina matumizi ya tasfida katika mahusiano ya kila siku kwa kuwa patakuwa na migongano na mitafaruku miongoni mwa wanajamii. Aidha malengo ya mawasiliano hayawezi kuafikiwa pasina upole.

### **3.5 Hitimisho**

Katika sura hii tumeelezea uhusiano baina ya upole na tasfida upole. Aidha tumeelezea upole kulingana na misimamo ya wataalum mbalimbali. Tumejadili mitazamo ya upole kama vile upole kama kaida ya kijamii, mkakati wa mazungumzo, mkataba wa mazungumzo na mtazamo wa kuokoa uso. Isitoshe tumechanganua tasfida mbalimbali katika nyimbo za harusi za lugha hizi mbili na kueleza jinsi zinavyotumika kuinga uso na kuendeleza upole miongoni mwa wanajamii. Tumegundua ya kwamba njia ya kuwa mpole zaidi ni kutumia tasfida katika mahusiano na mitagusano ya kila siku.

## SURA YA NNE

### UWIANO KATIKA TASFIDA ZA KISWAHILI NA EKEGUSII

#### 4.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu tumeshugulika nafasi ya tasfida katika kuendeleza upole katika Kiswahili na Ekegusii mtawalia. Katika sura hii tunashugulikia uwiano wa tasfida za Kiswahili na Ekegusii. Ulinganishi huu utatekelezwa kwa kuzingatia tasfida za lugha hizi mbili. Ikumbukwe kuwa lugha hizi mbili zina asili moja kwani zote zilitokana na Mame Bantu. Kwa hivyo kwa kiwango kikubwa zinawiana katika matumizi ya tasfida ili kuendeleza upole katika jamii. Hata hivyo hakuna lugha mbili zinazofanana katika kila hali. Ulinganishi huu pia unabainisha ni tasfida zipi zinazofanana na ni zipi zinazotofautiana kwa mujibu wa nadharia ya upole.

Katika kila mitagusano lazima kuwepo na ushirikiano na taratibu za kiuwiano ili kuhakikisha kwamba mawasiliano baina ya watu yanaendelea. Wazungumzaji wa Kiswahili na Ekegusii hutagusana katika shughuli zao za kila siku. Aidha mitagusano hii haiwezi kuendelea bila kutumia lugha ya upole. Mawazo haya yanawiana na ya Brown na Levinson wanaositisha kwamba upole ni muhimu katika mitagusano ya kila siku. Kwa hivyo tutaangazia lugha hizi mbili kwa kuzilinganisha na kuona ni tasfida zipi zinazofanana na ni zipi zinatofautiana. Ikumbukwa kwamba kila lugha ina tasfida zake. Kwa hivyo wazungumzaji wa Kiswahili na Ekegusii pia hutumia tasfida kuhifadhi uso na kuendeleza upole katika mawasiliano ya kila siku. Majukumu ya tasfida za lugha hizi mbili yanawiana kwa kiasi fulani. Ili kudhihirisha uwiano huo, tutangazia tasfida za Kiswahili na Ekegusii.

#### 4.1 Tasfida za Kiswahili na Ekegusii

Kiswahili ni lugha ambayo hutumiwa na watu wengi katika shughuli za kila siku. Kutokana na majukumu yake, lugha hii ina tasfida anuwai ambazo huundwa ili kutumiwa na wazungumzaji wake katika kuinga uso na kuendeleza upole katika mawasiliano. Wataalamu kama vile Harry (1954) ameeleza kwamba kila lugha huashiria mfumo jamii husika ambao hutawala lugha hiyo kimatumizi. Hata ingawa Ekegusii ni lugha ya kibantu kama ilivyo Kiswahili, lugha hizi zina tofauti zake licha ya kuwa

tasfida nyingi zinakaribiana. Hymes (2000) anasema kwamba kila jamii ina jumla ya mitazamo, kaida, malengo na maadili yanayoitambulisha kundi la watu. Mawazo haya yanasawiana na mawazo ya Franz Boaz (1978) ambaye pia anasema kwamba lugha inayotumiwa na watu wote katika jamii hubeba utamaduni wa watu hao.

Tungependa kuelezea kwamba Ekegusii kinadhihirisha kuwa tasfida zake zinaweza kufanana na za Kiswahili. Hata hivyo kuna baadhi ya tasfida zinazotofautiana kama anavyosema Illuman (2005) kwamba kila utamaduni huwa na mambo ambayo hayazungumzwi wazi. Hii ni kwa sababu kuna tasfida nyingi katika Ekegusii zinazofanana na zile za Kiswahili. Kwa hivyo tasfida hutumika ili kukwepa usemi unaosababisha taharuki na migongano baina ya watu. Tutachanganua kwa kulinganisha tasfida zilizotumika katika nyimbo za harusi za Kiswahili na Ekegusii kurejelea mada mbalimbali kama ifuatavyo:

#### 4.1.1 Tasfida za kujamiiiana

Kujamiiiana ni mada ambayo imepewa tasfida nyingi kwa kuwa ni mwiko. Ni mada ya mwiko ambayo huleta aibu miongoni mwa watu na huwa haitajwi hadharani. Ili kuficha aibu ya kutumia maneno ya mwiko, wasemaji hutumia tasfida kutaja kitendo cha kujamiiiana hadharani bila kuvunja au kuvuruga mawasiliano. Kwa hivyo nyimbo za harusi za Kiswahili zimesawiri tasfida zifuatazo kurejelea mada ya kujamiiiana: kuonana, kukutana, kushirikiana, na kujuana.

Tasfida zifuatazo pia zimedhihirika katika nyimbo za harusi za Ekegusii kurejelea kujamiiiana:

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Kororana	kounana	ngono
Koumerana	kukutana	kukutana
Koruga	kupika	kupika
Korara	kulala	kulala
Koba amo	kuwa pamoja	kushiriki ngono
Koria endagera	kula chakula	kuchumbiana
Komanyana	kujuana	kujuana

Koboera	kufunga	kufanya ngono
Kobwaterana	kushirikiana	kushiriki ngono
Korwana	kupigana	kupigana
Goitana	kupimana	kupigana
Konywa amache	kunywa maji	kukata kiu

Tasfida kuonana, kujuana, kula na kulala ni maneno ya kawaida katika lugha. Kwa hivyo maneno hayo yanapotumika huwa yana upole zaidi kuliko neno halisi. Aidha maneno hayo hayasababishi uchukivu wala kukwamza mawasiliano. Kwa hivyo wanajamii huyatumia kama njia ya kuinga uso kutokana na aibu inayoletwa na kitendo hicho.

Tasfida hizi za kujamiiana hutumika kusitiri uso na pia hutekeleza majukumu ya kuendeleza upole miongoni mwa wanajamii. Maneno kuonana, kujuana na kukutana yanapotumika huonekana ya kawaida na kwa hivyo hayawezi kudhuru uso wala kukwamiza mawasiliano. Kujamiiana nje ya ndoa pia huchukuliwa kuwa ni mwikokatika jamii, kwa hivyo huwa ni kinyume cha maadili ya wanajamii. Tasfida kama vile kibiritingoma, kahaba na kiberenge na kiruka njia hutumika kurejelea kujamiiana nje ya ndoa. Tasfida hizi hutumika ili kuinga nyuso za wahusika.

Kutokana na mifano ambayo tumeorodheasha hapo juu, ni kwamba tasfida za kujamiiana zipo katika nyimbo za harusi za lugha zote mbili. Ni dhahiri kwamba mada ya kujamiiana imepewa tasfida nyingi katika lugha zote mbili. Uwiano upo kwa upeo mkubwa. Tofauti iliopo ni kwamba kuna baadhi ya tasfida zinazotumika kurejelea mada ya kujamiiana katika Ekegusii ambazo hazipo katika lugha ya Kiswahili.

#### **4.1.2 Tasfida za sehemu za siri za mwili**

Baadhi ya sehemu zote za mwili ni mwiko kutajwa hadharani. Kwa hivyo kuna baadhi ya sehemu za mwili ambazo hutajwa vile zilivyo na sehemu zingine hutasfidiwa kwa



kuwa ni mwiko na hazitajwi kwa njia ya moja kwa moja miongoni mwa wanajamii. Hii ni kwa sababu zinaleta aibu.

Sehemu ambazo hutasfidiwa ni kama vile siri ya mke na siri ya mume, makalio na matiti. Tasfida hizi hutumika kutajia sehemu hizo kwa lengo la kukinga uso na kudumisha heshima baina ya watu. Sehemu za siri ya mume na mke ni mwiko miongoni mwa wanajamii. Kwa hivyo tasfida hutumika kutaja sehemu hizi ili kukwepa aibu.

Tasfida zinazotumika kurejelea sehemu ya uume katika Kiswahili ni kama vile mkuki, mchi, mpini, bunduki, mshale, fimbo, kalamu, musumeno na mtaimbo miongoni mwa tasfida nyingi zinazotumika. Tasfida hizi zimedhihirika katika nyimbo za harusi za Kiswahili.

Katika nyimbo za harusi za Ekegusii tasfida ambazo zimedhihirika kurejelea siri ya mume ni kama zifuatavyo:

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Omogoye	kamba	kamba
Ritimo	mkuki	mkuki
Enguba	ngao	ngao
Omoswago	kitwangio	mchi
Ekebago	mti wa shoka	mpini
Omosumeno	msumeno	musumeno
Omotarimbo	mtaimbo	mtaimbo
Enyimbo	kijiti	fimbo

Kwa kuwa siri ya mume ni mwiko, tasfida hizi hutumika kukinga nyuso za wanajamii katika mawasiliano. Aidha zinatumika kuendeleza na kudumisha upole katika mawasiliano.

Siri ya mke pia imepewa tasfida nyingi katika lugha za Kiswahili na Ekegusii. Tasfida zinazotumika katika nyimbo za harusi za Kiswahili ni kama vile: shamba, boma, kisima, ziwa, chombo, mizigo, kanisa, kitu na chakula miongoni mwa tasfida zingine. Tasfida hizi hutumika kwa lengo la kuokoa uso wa wanajamii kutokana na aibu inayosababishwa na sehemu hii ya mwili.

Tasfida hizi pia zimedhihirika katika nyimbo za harusi za Ekegusii kureejelea siri ya mke kama ifuatavyo:

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Omochie	boma	boma
Endagera	chakula	chakula
Enyomba	nyumba	nyumba
Egesima	kisima	kisima
Richambe	mkeka	kitanda
Omogondo	shamba	shamba
Ekonu	kitwangio	kinu
Enka	makao	familia

Maneno yanayohusu sehemu za siri husababisha aibu na uchukivu miongoni mwa wanajamii yanapotajwa moja kwa moja. Kwa hivyo tasfida zinapotumika huendeleza upole na kuhifadhi nyuso za kibinafsi na nyuso za hadharani za wanajamii. Tasfida hizi hutumika kuokoa uso wa mke na pia kuendeleza upole katika mawasiliano baina ya watu. Aidha tasfida zinatumiwa ili kuhakikisha kwamba malengo ya mawasiliano yameafikiwa.

Kutokana na mifano ambayo tumetoa hapo juu ni dhahiri kwamba tasfida za sehemu za siri zipo katika lugha zote mbili. Tumetambua kwamba sehemu za siri za binadamu zimepewa tasfida nyingi katika lugha hizi na tasfida hizo zinakaribina kwa kiwango kikubwa.

#### **4.1.3 Tasfida za kumtaja mke**

Katika mitagusano ya kila siku, upole unahitajika baina watu ili kuendeleza shughuli zao za kila siku bila mitafaruku wala kuwavunjia watu wengine heshima zao. Katika hali hii watu huitana majina mbalimbali kulingana na uhusiano baina yao. Katika nyimbo za harusi za Kiswahili tasfida zifuatazo zimedhihirika kumtaja mke, Picha, dhahabu, zawadi, mpenzi chakula na kipato. Hutumiwa na mume kumtaja na kumsifia bibi harusi katika siku yake ya arusi.

Nyimbo za harusi za Ekegusii pia zimedhihirisha tasfida zifuatazo:

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Omotangi	wa kwanza	kifungua mimba
Omwanchi	anayependa	kipenzi
Omogisangio	mshirika	rika
Yuu	rafiki	mpenzi
Amaguta	mafuta	manukato

Kutokana na mifano ambayo tumetoa hapo juu, ni dhahiri kwamba tasfida za kumtaja mke zipo katika za lugha za Kiswahili na Ekegusii. Tofauti ni kwamba maneno yanayotumika kurejelea tasfida hizi hutofautiana katika lugha hizi mbili.

#### **4.1.4 Tasfida za ujauzito**

Ujauzito umepewa tasfida pia kwa kuwa ni mwiko miongoni mwa wanjamii. Katika lugha ya Kiswahili tasfida kama vile mjamzito hutumika kurejelea mimba. Tasfida amejifungua na amepata mgeni hutumika kurejelea kujifungua. Hata hivyo hazijabainika wazi katika nyimbo za harusi za kiswahili. Katika Ekegusii tasfida za ujauzito zimeanishwa katika vitengo viwili. Kwanza wakati mama ni mjamzito na pili wakati mama amejifungua. Kwa hivyo tasfida zifuatazo zimebainika katika nyimbo za harusi za kurejelea mada ya ujauzito.

Tasfida zifuatazo hutumika kurejelea mimba katika Ekegusii:

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Nare noborito	ana mzigo	mjamzito
Kwebwaterania	kushikana	ana mimba
Orosire	amechoka	ana mimba
Gosimeka	kupanda	mjamzito

Katika Ekegusii Tasfida zifuatazo pia hutumika kurejelea kuzaa:

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Gokonyeka	kusaidika	kusaidika
Korwa omote igoro	kutoka juu ya mti	kujifungua
Konyora omogeni	kupata mgeni	kupata mgeni
Kogongia	kunyonyesha	kujifungua

Tasfida hizi hutumika kuonyesha upole hasa kwa kuzingatia kwamba mama akiwa mjamzito yumo hatarini. Pia zinatumiwa kukinga uso wa mama mamzito. Aidha wanajamii huzitumia tasfida hizi kama njia ya kuonyesha upole kwa mama mjamzito.

Tasfida za ujauzito hutumika kama njia ya kuficha na kusitiri uso wa mama mjamzito akiwa na mimba na baada ya kujifungua. Tasfida kama vile kupata mgeni na kusaidika ni maneno ya kawaida katika lugha ambayo hayana uchukivu wowote yanapotumika katika mawasiliano ya kila siku.

Kutokana na mifano ambayo tumutoa ni dhahiri kwamba tasfida za ujauzito hutumika katika lugha za Kiswahili na Ekegusii. Tofauti iliopo ni kwamba Ekegusii kimedhihirisha tasfida anuwai zitumiwazo kurejelea ujauzito.

#### **4.1.5 Tasfida za mapenzi**

Mapenzi pia yamepewa tasfida katika lugha za Kiswahili na Ekegusii. Tasfida zifuatazo zimebainika katika nyimbo za harusi za lugha hizi mbili. Katika Kiswahili tasfida kama vile maradhi, na mito zimetumika kurejelea mapenzi. Ekegusii pia kimedhihirisha tasfida zifuatazo:

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Obwanchani	kupenda	kupendana
Enyangi	harusi	kipenzi
Amariga	machozi	machozi

#### **4.1.6 Tasfida za majina ya kijamii**

Nyimbo za harusi za Ekegusii zimedhihirisha tasfida ya majina ya kijamii ilihali tasfida hizo hazipo katika nyimbo za harusi za Kiswahili.

Tasfida ambazo zimedhirika katika Ekegusii ni kama zifuatazo:

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Mogisangio	mshirika	rika
Abagaka	wanaume waliokomaa	wazee
Mosamba mwaye	aliyechoma kwake	mtoto aliyezaliwa
Moisia	mvulana	mvulana
Omongwana	muungwana	mume
Baba	mama mzazi	mama

Tasfida za majina ya kijamii hutumika kuonyesha upole katika mahusiano. Hii ni kwa sababu inaaminika kwamba ni mwiko kwa mtoto kuwaita wazazi wake majina halisi. Aidha wanajamii wanaamini kwamba kuwaita wakwe, bayvaa, mavvaa, mkazamwana miongoni mwa majina mengine kwa majina yao ni ukosefu wa upole. Kwa hivyo inawabidi kutumia maneno ya heshima kuendeleza upole. Tasfida hizi pia hudhihirika katika nyimbo za harusi za Ekegusii.

Kutokana na mifano ambayo tumetoa hapo juu, ni kwamba tasfida za majina ya kijamii zimedhihirika katika nyimbo za Ekegusii. Tumetambua kwamba tasfida hizo hazipo katika nyimbo za harusi za Kiswahili. Katika hali hii tunaweza kusema kwamba kila lugha ina njia za kuteua tasfida na tasfida hizo hutumika kwa njia ya kipekee. Aidha tasfida hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine.

#### **4.1.6 Tasfida za mahusiano**

Mahusiano mema ni muhimu miongoni mwa wanajamii. Ili kudumisha mahusiano haya, wanajamii hutumia tasfida. Nyimbo za harusi za Ekegusii zimedhihirisha tasfida zifuatazo:

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Mogisangio	mshirika	rika
Yuu	rafiki	rafiki
Iso	baba	baba
Baba	mama	mama
Moisia	mvulana	mvulana

Kutokana na tasfida hizo tulizorodhesha, ni bayana kwamba lugha hizi mbili zina mada ambazo zimetasfidiwa katika nyimbo za harusi kama vile kujamiiana, mapenzi, na sehemu za mwili miongoni mwa mada zingine. Kwa kuwa tasfida ni kipengele cha lugha ambacho huumbwa na utamaduni, wanajamii hukuza maadili na kuendeleza heshima zao kupitia kwa nyimbo kwa sababu zina wingi wa matumizi ya tasfida. Aidha wanazitumia kukuza mahusiano mema baina yao katika mitagusano ya kila siku. Ikumbukwe kwamba haya ni maneno ambayo hupatikana katika diskosi ya kijamii na kukubalika na wanajamii ili kutumika kwa lengo la kuhifadhi nyuso na kuendeleza upole katika mawasiliano.

#### 4.2 Ulinganishi naulinganuzi wa tasfida za Kiswahili na Ekegusii

Kutokana na tasfida ambazo tumeorodhesha imeabainika kuwa katika lugha zote mbili mada ya kujamiiana na sehemu za siri zimepewa tasfida nyingi ambazo hukaribiana. Lugha hizi mbili ni za asili moja. Kwa hivyo kwa kiwango kikubwa zinawiana katika matumizi ya tasfida. Kwa kuwa hakuna lugha mbili zinazofanana kikamilifu pana tofauti chache za hapa na pale. Tasfida zinazofanana katika lugha zote mbili zinadhihirika katika mifano ifuatayo:

Tasfida za kujamiiana

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Kororana	kuonana	kuonana
Komanyana	kujuana	kujuna
Koboera	kufungia	kujuana
Koumerana	kukutana	kukutana

Tasfida za seshemu ya siri ya mume:

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Ritimo	mkuki	mkuki
Omoswago	kitwangio	mchi
Ekebago	mti wa shoka	mpini
Omosumeno	msumeno	musumeno
Omotarimbo	mtaimbo	mtaimbo

Enyimbo	kijiti	fimbo
---------	--------	-------

Tasfida za sehemu ya siri ya mke:

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Endagera	chakula	chakula
Enyomba	nyumba	nyumba
Egesima	kisima	kisima
Omogondo	shamba	shamba

Imebainika kuwa sehemu za siri za mke na mume zimepewa tasfida nyingi katika lugha zote mbili. Hii ni kwa sababu kutaja sehemu za hizo moja kwa moja ni mwiko na kwa hivyo hazitajwi hadharani. Hata hivyo si sehemu zote za mwili zinazoleta aibu miongoni mwa wanajamii. Hii ni kwa sababu neno ambalo ni aibu katika jamii moja huenda si la aibu katika jamii nyingine. Aidha sehemu zingine za mwili hutajwa moja kwa moja katika lugha fulani ilihali sehemu hizo hizo lazima zitafutiwe tasfida katika lugha nyingine. Mada zingine ambazo zimepewa tasfida kulingana nyimbo za harusi ambazo tumetalii ni zile zinazorejelea mapenzi na mke.

Ulinganifu umeonekana kwa upeo kwa kuzingatia tasfida hizi. Hata hivyo kuna baadhi ya tasfida ambazo zinazotofautiana. Tumetambua kwamba maneno mengine yanayoashira mahusiano katika nyimbo harusi za Kiswahili yanatumika vile yalivyo bila kutasfidiwa ilihali maneno hayo hayo katika nyimbo za harusi za Ekegusii lazima yatafutiwe tasfida kama inavydhihirika katika mifano ifuatayo ya tasfida za mahusiano:

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Abagaka	wanaume waliokomaa	mzee
Moisia	mvulana atakayea	mvulana
Baba	mama	mama
Yuu	rafiki	mpenzi
Omwanchi	anayependa	mke/mume

Nyimbo za harusi za Ekegusii zimedhihirisha tasfida za majina ya kijamii ambazo hazipo katika nyimbo za harusi za Kiswahili.

Mifano ya tasfida hizo ni kama zifuatavyo:

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Mogisangio	mshirika	rika
Abagaka	wanaume waliokomaa	wazee
Mosamba mwaye	aliyechoma kwake	mtoto aliyezaliwa
Moisia	mvulana	mvulana
Omongwana	muungwana	mume

Nyimbo za harusi za Ekegusii zimedhihirisha tasfida za kuzaa ambazo hazijabainika katika nyimbo za harusi za Kiswahili. Tasfida hizo ni kama zifuatavyo:

<i>Ekegusii</i>	<i>tafsiri</i>	<i>Kiswahili</i>
Gokonyeka	kusaidika	kujifungua
Korwa omote igoro	kutoka juu ya mti	kujifungua
Kogongia	kunyonyesha	kujifungua

Kutokana na mifano ambayo tumetoa ni dhahiri kwamba hakuna lugha zinazofanana kikamilifu kwa kila hali. Kwa hivyo tunaweza kudai kwamba maneno au usemi fulani ambao ni upole katika tamaduni moja huenda ikawa ni utovu wa upole katika tamaduni nyingine. Aidha kuna baadhi ya mambo kama vile kujamiiana, sehemu za mwili, mapenzi, ujauzito mke, majina ya kijamii na mahusiano ambayo hutasfiwa kwa lengo la kukinga uso na kuendeleza upole miongoni mwa wanajamii. Imebainika kwamba katika Kiswahili majina ya na mahusiano hutajwa vile yalivyo bila kutasfiwa na katika Ekegusii lazima yatafutiwe tasfida.

Tasfida zina majukumu ya kimsingi katika jamii. Kwa hivyo huzuia uwezekano wa kuzuka kwa migongano mitafaruku miongoni mwa wawasilianaji. Tasfida pia huhuzishwa na kaida na maadili ya kitamaduni ambayo hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Aidha vitendo vinavyotishia uso na mikakati ya upole hutofautiana katika tamaduni zote. Kwa hivyo matumizi ya tasfida hutofautiana kwa kutegemea utamaduni wa jamii husika. Hata hivyo imebainika kwamba tasfida nyingi za Kiswahili na Ekegusii



zinawiana kwa upeo mkubwa. Hii ni kwa sababu lugha hizi zina asili moja. Kutokana na hali hii ni dhahiri kwamba tasfida zipo katika kila lugha na hutumika kwa njia ya kipekee. Licha ya madai kwamba tasfida za Kiswahili hukaribiana na tasfida za Ekegusii ikumbukwe kwamba hakuna lugha mbili zinazofanana katika kila hali.

#### **4.8 Hitimisho**

Katika sura hii tumeshugulikia uwiano wa tasfida za Kiswahili na Ekegusii. Aidha tumebainisha tasfida zinazopatikana katika kila mojawapo ya lugha hizi na zile ambazo zinatofautiana. Tumetambua kwamba tasfida za kujamiiana na tasfida za sehemu za siri ya bindamu, miongoni mwa tasfida zingine zipo katika lugha zote. Vile vile tumegundua kwamba tasfida za mahusiano na tasfida za kijamii hazijadhihirika katika nyimbo za harusi za Kiswahili. Aidha tumegundua kwamba kuna maneno katika lugha ya Ekegusii ambayo lazima yatafutiwe tasfida na maneno hayo hayo hutajwa vile yalivyo katika lugha ya Kiswahili lakini bado yanadumisha upole pasipo bila kuvuruga wala kukwamiza mawasiliano. Pia tumetambua kwamba kuna baadhi ya tasfida zilizotumika katika lugha ya Kiswahili ambazo zipo katika lugha ya Ekegusii. Tunachotaka kusistiza ni kwamba ni kweli kila lugha asilia ina tasfida zake zisizoweza kutumika au kulazimishwa katika lugha nyingine. Kwa mfano, Ekegusii kinadhihirisha tasfida za mahusiano na tasfida za majina ya kijamii ambazo hasijadhihirika katika nyimbo za harusi za Kiswahili.

## SURA YA TANO HITIMISHO

### 5.0 Utangulizi

Tulidhamiria kuchunguza uwiano wa tasfida za Kiswahili na Ekegusii kama mkakati wa upole. Ili kuafikia malengo yetu, ilitubidi kudurusu kazi mbalimbali ambazo zimetuwezesha kufikia hatua hii. Kwa hivyo katika sura hii tunatoa muhtasari wa utafiti wetu. Pia tutatoa mapendekezo kwa manufaa ya tafiti zitakazofanywa baadaye kuhusu suala la tasfida kama mkakati wa upole katika shughuli zingine au lugha zingine. Tumetambua kwamba utamaduni wa jamii yeyote ile unaingiliana na kuambatana na mfumo wa jamii hiyo. Kwa hali hii lugha ndiyo hutumika kufafanulia itikadi, imani na kuendeleza upole wa jamii husika. Jambo hili pia hufanikishwa kupitia maingiliano ya watu ambao hutumia tasfida. Isitoshe, utamaduni wa watu fulani, jinsi unavyohusiana na mazingira ambamo watu hao wanaishi, hujielezea kupitia kwa lugha yao tasfida zikiwemo. Kwa vile hakuna jamii mbili zinazolingana na kuwa sawa kitamaduni, mara nyingi huwa ni vigumu lugha moja kueleza kikamilifu dhana iliyo katika lugha nyingine. Ni katika hali hii, lugha hulazimika kukopa maneno kutoka lugha nyingine kwa minajili ya kueleza mambo mapya yanayopatikana katika lugha hizo. Tasfida kwa hivyo hutumika kudhibiti mahusiano na mitagusano ya kijamii. Aidha zinawawezesha watu kuishi kwa amani na kuwa na maingiliano bora katika mitagusano ya kila siku. Yaani ni kipengele cha lugha chenye upole ambacho hufanikisha mawasiliano. Isitoshe kuwepo kwa matumizi ya tasfida miongoni mwa wanajamii kunamaanisha kuwepo kwa upole katika jamii. Matumizi ya tasfida miongoni mwa watu ni ishara tosha ya kukwepa vitisho kwa uso au hata uchukivu baina ya watu. Aidha kipengele hiki cha lugha uhakikisha kwamba malengo ya mawasiliano yameafikiwa. Tasfida kama mojawapo ya mkakati wa upole hutekeleza majukumu ya kimsingi katika jamii ya kukabiliana na mitafaruku na migongano miongoni mwa watu katika mawasiliano.

### 5.1 Muhtasari wa matokeo

Utafiti huu ulijikita katika kujadili uwiano wa tasfida za Kiswahili na Ekegusii kama mkakati wa upole. Tasfida hizo zimedhihirika katika viwango vyote vya matumizi ya lugha. Kutokana na utafiti huu ni dhahiri kwamba haipotesia zetu zina mashiko. Kwa

hivyo hatuna budi kudai kwamba kuna tofauti zinazodhihirika baina ya tasfida za Kiswahili na Ekegusii. Mifano ya tasfida zinazotofautiana ni, tasfida za mahusiano, wadudu, wanyama, nanyakati miongoni mwa zingine. Tasfida hizo huathiri upole miongoni mwa wazunguzaji wa lugha za Kiswahili na Ekegusii.

Katika sura ya pili tuliweza kushugulikia hali zinazozua matumizi ya tasfida katika lugha hizi mbili na kuonyesha tasfida mbalimbali zinazopatikana katika kila lugha. Aidha tumeweza kuthibitisha kwamba tasfida zipo katika lugha hizi na hutumika kutegemeana muktadha ambamo wanajamii hujipata.

Lengo la kwanza la utafiti ambalo ni hali zinazozua matumizi ya tasfida liliafikiwa. Kama inavyojadiliwa katika sura ya pili, hali mbalimbali miongoni mwa wanajamii zinazua matumizi ya tasfida zimebainika ili kuokoa nyuso za watu na kuendeleza upole katika mawasiliano. Hali hizo kama zilivyopendekezwa na waasisi wa nadharia ya upole zimebainika katika uchunguzi huu katika lugha zote mbili. Aidha tumebaini kwamba kuna hali fulani katika Ekegusii zinazozua matumizi ya tasfida ambazo hazipo katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na uchunguzi huu ni dhahiri kwamba tasfida zote haziwezi kufanana katika kila lugha kwa kuwa kila lugha hutumia tasfida kwa njia ya kipekee.

Katika sura ya tatu, tumechanganua mchango wa tasfida za Kiswahili na Ekegusii katika kuendeleza upolena kukinga uso ambapo tulipata tofauti pale ambapo neno laweza kuwala upole katika Kiswahili ilihali neno hilo hilo si la upole katika Ekegusii. Vile vile tumetambua kwamba si maneno yote ambayo ni mwiko katika Kiswahili yanaweza kuwa ni mwiko katika Ekegusii. Hii ni kwa sababu kila watumizi lugha wana mila, dseturi na itikadi tofauti zinazoelekeza jamii hiyo. Ilibainika kwamba kila utamaduni tasfida zake na utamaduni huo una mbinu za kuteua maneno yanayokubalika na wanajamii kuwa ni mwiko. Aidha tasfida hizo hutumika kwa njia ya kipekee. Isitoshe tumebaini kwamba tasfida zipokatika lugha hizi mbili. Kutokana na hali hii ni dhahiri kwambaneno ambalo ni la tasfida katika lugha moja huenda si tasfida katika lugha nyingine. Hata hivyo tofauti za hapa na pale zimedhihirika na tofauti hizo huchangia

kukuza mahusiano, na kuendeleza upole baina ya wazungumzaji wa lugha hizi katika mawasiliano.

Katika sura ya nne, tumelinganisha tasfida za Kiswahili na Ekegusii. Tumetambua kwamba tasfida nyingi za Kiswahili na Ekegusii zinakaribiana kwa kiwango kikubwa katika kuendeleza mawasiliano. Katika haipotesia yetu ya mwisho tumegundua kwamba kuna tofauti kiasi baina ya tasfida za Kiswahili na Ekegusii hasa pale ambapo mada fulani hutasfidiwa katika Ekegusii na hasijapewa tasfida katika Kiswahili. Aidha maneno mengine hutajwa vile yalivyo katika Kiswahili na katika Ekegusii lazima yatafutiwe tasfida. Hata hivyo tasfida katika lugha zote mbili huchangia kuendeleza upole miongoni mwa wanajamii. Kutokana na hali ni dhahiri kwamba tasfida ni chombo ambacho hutumika kuongeza na kuendeleza upole katika mitagusano ya kijamii.

Nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1978, 1987) ilitufaa katika kazi hii hasa katika kuchunguza tasfida za Kiswahili na Ekegusii na jinsi tasfida hizi zinavyoshugulikia kuendeleza upole miongoni mwa wanajamii. Utafiti wetu umebaini kwamba kazi ya aina hii kuhusiana na ulinganishaji wa tasfida za Kiswahili na Ekegusii kama mkakati wa upole haijafanyiwa uchunguzi kwa kuwa kuna uchukulizi kuwa lugha hizi zina tasfida ambazo hazijabainishwa vilivyo miongoni mwa mazungumzaji wa Kiswahili na Ekegusii.

Utafiti huu umetambua kwamba lugha hizi zina matumizi mengi ya tasfida miongoni zinazorejelea mada mbalimbali. Pia wazungumzaji wa lugha hizi hutumia Kiswahili katika shughuli zao za kila siku. Kutokana na hali hii ni kwamba kuna mitagusano baina ya wazungumzaji wa lugha Kiswahili na Ekegusii. Jambo hili laonyesha kwamba katika mitagusano, wazungumzaji wanahitaji kuchukua tahadhari wanapotumia lugha ambazo si lugha zao za kwanza ili kuepuka mitafaruku baina yao na pia kudumisha upole katika mawasiliano. Uchunguzi wetu umebainisha kuwa tasfida ni kipengele muhimu cha lugha ambacho hutumika kuongeza na kuendeleza upole katika mawasiliano. Kwa hivyo wazungumzaji wa lugha hizi hujali mahitaji ya nyuso za washiriki wa mawasiliano. Wanatumia tasfida kama mbinu ya kuendeleza upole na kukabiliana na vitendo

vinavyotishia nyuso. Yaani tasfida hutumika kama njia mbadala ya kuendeleza upole miongoni mwa wanajamii. Hivyo basi tunadai kwamba tasfida ni mkakati wa upole wa kuokoa nyuso za wanajamii.

Imebainika kwamba watu huwa wapole katika mawasiliano kupita kwa matumizi ya tasfida. Hii ni kwa sababu tasfida ni matumizi ya lugha isiyo ya moja kwa moja na zimehusishwa na mkakati wa kuwa nje ya rekodi. Kutokana na hali hii, ni kwamba tasfida huchukua nafasi kubwa katika kuendeleza upole katika mawasiliano baina ya watu. Kama tulivyoelezea hapo awali, kipengele cha tasfida huongeza upole katika mawasiliano ya kila siku wakati kunaposhuka vitisho vya uso. Vile vile tumetambua kwamba tasfida, uso na upole ni mambo ambayo hayawezi kutenganishwa kamwe. Aidha kujua lugha sio kujua sarufi, bali pia ni kujua upole.

## **5.2 Mapendekezo**

Utafiti huu huwezi kudai kwamba umeshughulikia tasfida zote za Kiswahili na Ekegusii kikamilifu. Tunatarajia kwamba tafiti nyingi zitaweza kutalii masuala ya matumizi ya tasfida kama mkakati wa upole katika nyanja mbalimbali. Ni matumaini yetu kwamba wasomi wanaotumia lugha za Kiswahili na Ekegusii watatilia maanani suala la upole katika mawasiliano ya ana kwa ana au hata katika maandishi. Hasa kwa kutumia tasfida kama njia ya kuweka misingi thabiti ya kuokoa nyuso za watu za hadhrani na za kibinafsi. Pia watatumia tasfida kuendeleza na kudumisha upole katika mahusiano ya kila siku ili kupunguza mitafaruku na migongano baina ya wanajamii katika mawasiliano. Utafiti wetu ulijibana katika matumizi ya tasfida kama mkakati wa upole katika lugha mbili pekee. Kwa hivyo utafiti zaidi unaweza kufanywa katika lugha zingine kuhusu ulinganishi wa matumizi ya tasfida katika jamii tofauti kwa kutumia nadharia zingine.

## MAREJELEO

- Allan, K & Burridge, K. (1991). *Euphemism and Dysphemism*. New York. Oxford University Press.
- Brown, P. & Levinson, S. (1978). *Politeness! Some Universal in Language Usage*. Cambridge University Press.
- Brown, P.& Levinson, S (1987) . *Universals in Language Use: politeness phenomena*. In E .N Goody (ed.) *Questions and politeness*. Cambridge University Press.
- Fraser, B. (1990) *Perspectives on Politeness. I Journal of Pragmatics*.
- Fromkin, V. na Rodman, R. (1998). *Introduction to Languages*, Hoit. Reinchart and Winson.
- Gatambuki, M.G (2010). *A Cognitive Linguistic Analysis of Gikuyu Euphemism*. Tasnifu ya shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).
- Goffman, E. (1959). *The Presentation of Self in Everyday Life*. New York: Anchor Books.
- (1967). *The Presentation of Self in everyday life*: Basic Books new York.
- (1971). *Relations in Public*. Microstudies of the public Mordern Basic Books New York.
- Grice, H.P. (1975) *Logic and Conversations*. In Peter Cole & Jerry Morgan (eds.) *Syntax and Semantics*. New York, N.Y: Academic Press.
- Guthrie, M. (1954). *Classification of Bantu Languages*: London International African Institute Press.
- Harry, H. (1954). *Language in Culture*. Chicago Press.
- The University of Chicago Press.[http: www.netjeff. Com./humor /item.cgi](http://www.netjeff.com/humor/item.cgi).

- Hymes, D. (1964). *A Language, culture and society*. Newyork: Harper and Row publishers.
- Iribe, P. (2011) *Isimujamii*. Nairobi. Phoenix Publishers.
- Johnstone, B. (2008). *Discourse Analysis*. Meldon, M A, USA: Blackwell Publishing
- Kent, P. (1978). *Encyclopedia of Library and Information Science*. New York: Marcel Decker.
- Kothari, C. (2004). *Research Methodology*. (2<sup>nd</sup> edd) New Age Technology Press.
- Lakoff, R. (1973). *Logic of politeness: or minding your p's and q's*. Chicago Linguistic Society.
- Leech, G. (1983). *Principles of Pragmatics*. New York: Longman. Harcourt Brace.
- Levinson and Stephen C. (1983). *Pragmatics*. Cambridge: Cambidge University Press
- Marmaridou Sophia, S.A. (2000). *Pragmatics; Meaning of Cognition*, Amsterdam / Phillodephia: John Benjamin Publishing Company.
- Maricic, I. (2005). *Face in cyberspace: Facework (imp) politeness and Conflict in English Discussion Groups*. Goreborg: Vaxjo University Press.
- Mwebia, F. G. (2006). *A Lexical Pragmatic Analysis of Sense in Kimeru: Tasnifu ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi*. Haijachapishwa.
- Mukaria, J. M. (2011). *Misamiati ya Miiko na Tasfida katika Kiigembe*. Tasnifu ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Mutiso, K. (2005). *The Nature of Forbidden Language*. Tasnifu ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

- Nguti, M. (2013) *Ulinganishi wa matumizi ya tasfida za muktadha wa nyumbani katika Kikamba na Kiswahili*. Tasnifu ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Njeri, S. (2007). *Pragmatic Analysis of Gikuyu Lexical Euphemism in HIV / AIDS Discourse*: Tasnifu ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa
- Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi Jomo Kenyatta Foundations.
- Orodho,(2005). *Elements of Education and Social Sciences Research Methods*, Nairobi: Penguin Publishers.
- Trudgil, P. (2000). *Social Linguistic, An Introduction to Language and Society*. (4<sup>th</sup> edd) London: Macmillan Publishers Ltd.
- TUKI, (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam. TUKI.
- (2006). *English Swahili Dictionary* (Toleo la tatu) Dar es Salaam: TUKI.
- Wardhaugh, R. (2002). *Sociolinguistics. An Introduction to Language and Society* (4<sup>th</sup> edd.) London: Blackwell Publishers.
- Wambua R.S. (2009). *Variation in Dialectical Use of and Attitudes Towards Taboo Words and Euphemisms in Kikamba*. Tasnifu ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Methali*: Nairobi. Focus Books.
- Whitely W. (1969). *Swahili the Rise of a National Language*: Mthuen and Co. Ltd.
- Yule, G. (1996). *Pragmatics*. Oxford University Press.



## VIAMBATISHO

### Data ya uchanganuzi I: Nyimbo za harusi za Kiswahili

#### (1) UPendo

Furaha yangu arusi imetimia

Huyo ndiye wangu

Moyo ulomchagua,

Picha, dhahabu pembeni kulia,

Sasa hauna kulia,

Ni zawadi kwangu kutoka kwa mola,

Pendo limetimia

Mbele ya hadhira tumeshuhudiwa,

Kwa mengi mola ametutendea

Leo hadharani twalitangaza pendo letu,

Maana kwa imani tumetimiza pendo letu,

Mikono juu, vigelegele,

Jamani si ni raha hiyo,

Bila huyu siwezi,

Siwezi bila huyu

## (2) Sherehe

Sherehe hiyo, sherehe hiyo

Ya harusi imeshatimia

Wabariki mola kwa harusi yao

Ndoa ni furaha, sherehe hiyo

Sherehe ya harusi imeshatimia,

Tumefurahi si haba'

Ni harusi imefika

Sherehe hiyo ya harusi imeshatimia,

Sherehe ya harusi imeshatimia

Wameringakwa mahaba,

Wakiona la kushiba,

Kuolewa ni furaha

Sherehe hiyo ya harusi

Sherehe imeshatimia

Cheza cheza, leo umepata wako

Bibi arusi cheza, leo cheza

Cheza leo, umepata bwana

Cheza hatuna maneno, leo umepata bwana x2.

### (3) Ndoa

Kutizama hali ni jambo sawia,

Kwa walo tayari kuifunga ndoa

Ukiwa tajiri usioweza tulia,

Waweza tulia ukishapewa bibi bikira

Jambo la kuoa ni lenye fadhila,

Ila kwa kujua kumtukuza mola

Tamaa yako Ali ni yenye wasaa,

Kipato halali unategemea,

Maradhi ya mwili yaweza tulia,

Ukipata mwenye utakayemuoa

Iwapo fakili mnapokutana,

Chakula halali huwezi kutoa

Kwako hujali huwezi kumwambia,

Wewe si halali na mmefunga ndoa,

Salama harusi nendeni salama,

Mkae vizuri kwenye ndoa,

Nasi tu tayari kuwatembelea

Awape fadhili bila ya karaha,

Salama harusi nendeni salama

Mola awajalie mkae pamoja,

Kweli awajalie, mpate kivuli kisichofia

Salama harusi nendeni salama

#### (4) Upendo

Wakati wawili wanapooana,  
Wao ni sawa na mito miwiil inayokutana mahali pamoja,  
Ili kutengeneza mto mmoja,  
Maji haya hayawezi kuwa matulivu,  
Wakati wa mwanzo yanapokutana;  
Lakini kadiri yanavyoendelea kutiririka,  
Yatatulia kabisa oo aa

Maisha ya ndoa hufananishwa na safari ndefu,  
Lazima upitie kwenye ule mlima,  
Na kujipa moyoili ufikie upendo uliokomaa,  
Ili ufikie pendo hilo,  
Lazima ukubali kutuliza ndoa,  
Ili ndoa iwe nzuri sana.

Wakati wowote mwambie,  
Mpenzi wangu nakupenda tu aah,  
Hilo ndilo pendo,  
Mfanye mwenzi wako,  
Awe rafiki yako tena,  
Mweleze shida zako, mweleze hisia zako,  
Mweleze hitaji lako, mwambie kila jambo,

Furaha huwa nzuri katika ndoa,  
Mfurahie mwenzi wako wakati wowote,  
Mshirikiane, mwambie nakupenda,  
Mwone kama mmekutana mara ya kwanza,

Mwambie nakupenda

Mwambie wewe ni mzuri,  
Sikukosea kukuchagua wewe,  
Nakupenda mpenzi wangu,  
Nakupenda sana,

Upendo huvumilia, upendo hufadhili,  
Upendo hauchangamani, upendo haujivuni,  
Upendo hausababishi mabaya,  
Upendo hustahimili yote,

Mwambie mwenzako hitaji lako,  
Mwambie sitaki hili,  
Mwambie nahitaji hili,  
Mwambie kinachokuumiza roho,  
Hakika una usalama katika ndoa yako,  
Mpendane nyakati zote

### **(5) Harusi**

Harusi ni ya furaha kwa ndugu zetu,  
Wamefunga ndoa,

Wameamua kuwa kitu kimoja ee,

Mungu baba wabariki

Kama kristo alivyoipenda kanisa,

Ndivyo mme umpende mke wako,

Mke hapigwi kama gumbi gumbi,

Anatulizwa na maneno matamu

Nawe mke mtii mume wako,

Mpe heshima na kila kitu

Na mume naye atafurahi

Mshirikiane katika ndoa,

Naye Mungu atawabariki,

Awape amani

## Data ya uchanganuzi II: Nyimbo za harusi za Ekegusii

### (1) Kwaeri

Kwaeri Nyandego,

Bono nkogenda tore

Kwaeri Nyandego

Ee bono nkogenda tore

Kwaeri omongwana,

Bono nkogenda tore,

Kwaeri omongwana,

Chinsa chiaikire,

Kwaeri omwanchi one

Chinsa chiaerire,

Kwaeri omwanchi one

Ee bono nkogenda tore

Nachigotiria etiriri

Nkanyora nabuire

Kwaeri omongwana

Bono nkogenda tore

Nachigoteka ogoteka,

Nkanyora yanyure,

Kwaeri omongwana,

Bono nkogenda tore

*Tafsiri ya Kiswahili*

Kwaheri Nyandego,

Sasa tunaenda

Kwaheri Nyandego,

Ee sasa tunaenda

Kwaheri muungwana,

Sasa tunaenda,

Kwaheri muungwana,

Wakati umefika,

Kwaheri mpenzi wangu,

Wakati umefika,

Kwaheri mpenzi wangu,

Ee sasa tunaenda,

Nimerukaruka mchezo

Nimepata nimeshinda

Kwaheri muungwana

Sasa tunaenda

Nimeteka kuteka,

Nikapata imeingia

Kwaheri mpenzi

Sasa tunaenda



## (2) Mbwangonde

M'boera eee ee

M'boera bwango nde ng'ende

Ng'a omgoye mboere richambe

M'bwango nde eee

M'boera eeee

Richambe eeee

Omogoye ee ee

N'gende ee

N'sibera eee ee

N'sibera chinsa chiaikire,

Ng'a omogoye mboere richambe

## *Tafsiri ya Kiswahili*

Nifungie eee ee

Nifungie haraka nienda

Nipe kamba nifungie mkeka

Nina haraka ee

Nifungie eee

Mkeka ee

Kamba ee

Niende ee

Nifungie eee ee

Nifungie wakati umekwisha

Nipe kamba nifungie mkeka

(3) **Obwanchani**

Bwabokire, bwabokireobwanchani,

Bwabokire, bwabokire obwanchani

Bori bwakare, bori bwakare obwanchani

Bori bwa kare, bori bwakare obwanchani

Tema naende, tema naende torore

Tema naende, tema naende torore,

Ekeru narengi omwana obe nk'anigwa baba,

Obe nk'anigwa ee

Nk'anigwa timbasa koria amara a baba,

Timbasa koria amara ee

Nko'ria amara obe ng'a nintamue baba

Obe ng'a nint'amue ee

Ekeru nainyoi, tata agantebia,

Moisia gachi orisie,

Ndisia omobaso bwaira

Ngacha gotiga ee

Koria amara a baba,

Ngacha gotiga ee

*Tafsiri ya Kiswahili*

Umeanza upendo, umeanza upendo

Umeanza upendo, umeanzaupendo

Ule wa zamani, ule wa zamani upendo

Ule wa zamani, ule wa zamani upendo,

Jaribu tena, jaribu tena tuone

Jaribu tena, tuone jaribu tena

Nilipokuwa mtoto obe, nilikatazwa mama'

Obe, nilikatazwa,

Nilikatazwa nizile chango za mama,

Nizile change ee,

Nikila nitakuwa mtoro,

Obe nitakuwa mtoro

Nikikumbuka baba aliniambia,

Kijana, enda malishoni,

Naenda malishoni mchana kutwa,

Ndiposa nikaacha ee,

Nikaacha kula change za mama

#### **(4) Ekeru okegenda**

Osebe ekeru oregenda'

Ondangerie ngokobe

Switi switi banana,

Egetenga kieritoke

Abagaka inchuo tomane chimbe,

Erituko nario eri

Switi switi banana

Egetenga kieritoke

#### ***Tafsiri ya Kiswahili***

Osebe utakapoenda,

Uniite nikuzindikishe

Switi switi banana

Mgomba wa ndizi

Wazee njoo tuchukue mahari,

Siku ndio hii

Switi switi banana

Mgomba wa ndizi

#### **(5) Sirori**

(e)Sirori, sirori my dear

Engombe nyamagoro ane,

Sirori my dear

Nero yang'ura yuu?

Sirori my dear

Enyangi yomotangi

Naki ndakore morore?

Nere nkona korota,

Omwanchi twanchaine,

Baka enkoru ime

Twabangire enyangi

Enyangi yebitinge

Asibwe nebitinge

Ekeru togotara

Igo are maridadi

Naki ndakore morore?

Rituko erio rienyangi,

Naki ndakore morore ?

Rituko rienyangi,

Rituko nario rero,

Kindoche omwanchi one,

Are nomogoko

Ee ninde nomogoko,

Kori x2 kori maguta kori, x2

Kori maguta kori

Omosuko ntakorochi amariga akona goika

Narero iga oyee.

Omosuko ntakorochi amariga akona goika

Baba gachi mogondo,

Gosimeka chingende,

Nareroiga oyee,

Omosuko ntakorochi amariga akona goika

### *Tafsiri ya Kswahili*

Sirori, sirori my dear

Ng'ombe yenye miguu minne

Ndio imenipokonya mpenzi

Sirori, sirori mydear

Arusi ya kifungua mimba,

Nitafanyaje nimwone?

Ninamuota kila siku

Mpenzi tunapendana

Mpaka ndani ya roho

Tumepanga harusi

Harusi ya 'ebitinge'

Afungwe 'ebitinge'

Wakati tunapotembea

Anaonekana mrembo kweli

Nataka kumsalimia

Nitafanyaje nimwone?

Siku hiyo ya harusi

Nitafanyaje nimwone?

Siku ya harusi,

Siku ndio leo

Nkimwona mpenzi wangu,

Akiwa na furaha,

Ee nina furaha

Siku ndio leo

Kori kori mafuta Kori

Wakati sikuoni machozi yanidondoka

Mama enda shambani ukapande maharagwe

Na leo hivi oyee, wakati sikuoni,

Machozi yanidondoka